Ijumaa Desemba 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581882
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US
epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

UKURASA WA 2
**Mshtakiwa** kesi ya mihadarati adaiwa kuwa na vitambulisho viwili vya kupigia kura

UKURASA WA 3
**Korti** yaelezwa kocha wa Simba alivyopokea dawa kulevya, kuzitunza

UKURASA WA 4
**Madaktari** Tanzania wahudumia wagonjwa 2,770 kambi Comoro

UKURASA WA 22
**AMORIM ALIA UFITI WA WACHEZAJI MAN UNITED**

# Watoto wafukuzwa shule kisa wazazi wao wapinzani



• **Serikali** yawarejesha, mwalimu mkuu kikaangoni. Waziri Mkenda atoa tamko... *Endelea Ukurasa 2*



Wakazi wa Kijiji cha Miguruwe, wilayani Kilwa, mkoani Lindi, wakiangalia daraja lililosombwa na maji ya mvua mapema wiki hii na kukata mawasiliano ya barabara kati ya wilaya hiyo na Liwale. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 24
## SIMBA SC KAMILI, HAWAHOFII BARIDI

## Askari mbaroni madai ya kuua raia kwa risasi

UKURASA 4

# Toto Afya Kadi yarejeshwa

• **NHIF** yanasa wadanganyifu, warejesha bil. 15/- *Endelea Ukurasa 3*

**MICHEZO** YANGA YAFANYIWA FIGISU ALGERIA UK.24 **MAONI,** UK.6

# Mshtakiwa kesi dawa kulevya adaiwa kukutwa na vitambulisho viwili vya kura

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa Jamhuri katika kesi ya kusafirisha dawa za kulevya, Inspekta Msaidizi wa Polisi John Marwa, amedai kuwa alipompekua mshtakiwa Ally Jafari, alimkuta na vitambulisho mbalimbali vikiwamo viwili vya kupiga kura, vyote vikiwa na majina yake.

Inspekta Marwa alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati akitoa ushahidi mbele ya Jaji Godfrey Isaya.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ellen Masululi, alidai kuwa Machi 24, 2022 saa 10:00 alfajiri akiwa na askari wenzake, walifika Kituo cha Mabasi Mbezi kumkamata mtuhumiwa ambaye alifahamishwa anasafirisha dawa za kulevya.

"Nilitumiwa picha ya mtuhumiwa, namba ya basi analosafiria kwenda Tanga, la Tashrif lenye namba za usajili T 987 DLZ.

"Basi liliingia Kituo cha Magufuli Mbezi likitokea Sudan Temeke, lilipaki kwa ajili ya kupakia abiria wengine. Nilimfuata kondakta Ally Hussein nikamwamuru asipakie wala kushusha abiria hadi tumalize kazi yetu," alidai.

Marwa alidai kondakta alikubali na akiwa na afande Hassan, waliingia ndani ya basi kuanza kumtafuta mtuhumiwa. Walitumia picha waliyotumiwa na msiri wakafanikiwa kumkamata Iddi Nassoro kwenye kiti namba 37 na kushuka naye.

Inspekta Marwa alidai kuwa walipompekua, walimkuta na tiketi ya basi la Tashrif ikiwa na jina la Saidi Saidi, simu na pochi nyeusi ikiwa na dawa za kulevya.

Alidai kuwa dereva wa basi hilo, Andrew Paul, aliwafahamisha kuwa mshtakiwa alipandia Mwembe Yanga lakini kuna mwenzake Ally Jafari alipandia Sudan.

Shahidi alidai kuwa walirudi ndani ya basi kumtafuta Ally Jafari, walimpata alikuwa kakaa kiti namba 21 wakamshusha na kuanza kumpekua maungoni.

Alidai kuwa walimkuta na vitambulisho viwili vya kupiga kura vyote vinasoma jina lake, kitambulisho cha taifa, kadi ya Visa, kitambulisho cha makazi, tiketi na simu kisha alijaza vitu hivyo katika hati ya ukamataji mali.

Pia alidai kuwa alichukua maelezo ya dereva na kondakta kisha kuwaruhusu waendelee na safari wao wakaenda kufungua kesi Kituo cha Polisi Kimara.

Shahidi alidai alifunga kielelezo na saa 1:00 usiku na kukabidhi kwa Afande Neema na Machi 29, 2022 alikabidhiwa jalada kwa ajili ya kuendelea na upelelezi.

Aprili 4, 2022 alidai kuwa alipeleka simu za washtakiwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na Aprili 6, 2022 nilipokea taarifa ya uchunguzi kutoka Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhusu kielelezo kilichokamatwa.

"Nilikabidhi taarifa hiyo kwa mtunza vielelezo afande Neema na Juni 29, 2022 nilipokea taarifa kutoka Kitengo cha uchunguzi wa simu. Julai 13, 2022 nilikabidhi nyaraka mbalimbali zinazohusiana na hii kesi ikiwemo taarifa ya mkemia," alidai shahidi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Maliki Maliki, Iddi Nassoro, Ally Jafari na Mwinyi Mgazija. Wote wanashtakiwa kwa kufanya biashara ya dawa za kulevya aina ya heroine na walikamatwa Machi, 2022.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Mtambo wa kampuni ya mkandarasi wa ujenzi, ukitandaza lami katika eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanafunzi wafukuzwa kisa wazazi wapinzani

**Na Waandishi Wetu**

WANAFUNZI tisa katika Shule ya Msingi Izinga iliyoko Namanyere, Nkasi mkoani Rukwa, wamefukuzwa shule na wazazi kutakiwa kuwatafutia shule zingine za kuendelea na masomo yao.

Kwa mujibu wa barua zilizotolewa na mwalimu mkuu wa shule hiyo, hatua hiyo imechukuliwa kwa madai ya wazazi wao kutoa kashfa dhidi ya walimu na pia ni wafuasi wa upinzani.

Wakati wanafunzi hao wamefukuzwa, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imetangaza kuwarudisha huku ikitangaza kuchukua hatua za kiutawala dhidi ya mwalimu mkuu huyo baada ya uchunguzi kukamilika.

Katika mitandao ya kijamii jana, kulisambaa barua zinazodaiwa kuandikwa na mwalimu mkuu wa shule hiyo kwenda kwa wazazi pamoja na majina ya wanafunzi hao kutoka madarasa tofauti akiwamo wa darasa la kwanza.

Sehemu ya barua hizo zenye tarehe ya juzi, inaeleza sababu kuwa ni kutokana na kashfa na kauli mbaya ambazo mzazi husika alizitoa Novemba 27, mwaka huu, wakati wa mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Barua hiyo inaeleza kwamba kutokana na vitisho na dharau dhidi ya walimu, wameona hawana uwezo wa kufundisha watoto wao na kuwataka wakatafute shule nyingine.

**MSIMAMO WA SERIKALI**

Akitoa ufafanuzi kuhusu sakata hilo jana, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema kutokana na uamuzi huo alionita wa ajabu na ulioibua hisia tofauti, serikali itachukua hatua stahiki baada ya kukamilika uchunguzi na kupokea ripoti ya timu ya wadhibiti ubora wa elimu.

Alisema kama jambo hilo litabainika kuwa la kweli, litakuwa la ajabu na la kusikitisha kwa kuwa hakuna mwongozo wala sheria kwamba mwanafunzi atengwe kwa sababu ya mlengo wa kisiasa wa baba yake.

"Ni kweli mimi nimeona hizo taarifa zinasambaa kwamba kuna watoto wamefukuzwa shule kwa sababu wazazi wao ni wanachama wa CHADEMA (Chama cha Demokrasia na Maendeleo).

"Tunafuatilia tujue ukweli wa taarifa hizi; tayari timu ya wadhibiti ubora inaelekea kwenye shule hiyo. Kwa hiyo tutapata ukweli wa jambo hili baadaye.

"Lakini pamoja na kila kitu, ninapenda kusisitiza kwamba, shule zinaongozwa kulingana na miongozo, kulingana na sheria na taratibu ambazo zinawekwa na haiwezekani mwalimu mmoja ajitungie sheria zake mwenyewe. Vyama vya siasa vipo kwa mujibu wa sheria. Hakuna mwongozo wala sheria kwamba, mwanafunzi atengwe kwa sababu ya mlengo wa kisiasa wa baba yake," alisema.

Waziri Prof. Mkenda alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza hata mabinti waliopata mimba, ujauzito warudishwe shuleni.

"Sembuse watoto wa wazazi ambao kwa hiari yao wamechagua chama chochote cha kisiasa kuwa wanachama na vyama hivi vimesajiliwa kisheria?" alihoji.

Prof. Mkenda alisema hakuna ubaguzi kwa mtoto yeyote Mtanzania, hivyo kila mmoja anatakiwa kusoma shule kwa kuwa serikali inajenga shule nyingi na maelekezo ya Rais Samia ni kwamba, kuhakikisha kila mtoto anasoma.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Kwa mujibu wa barua iliyotolewa baadaye jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Nkasi, Afraha Hassan, hatua ambazo wamechukua ni pamoja na kuwarejesha shuleni wanafunzi wote tisa waliosimamishwa.

"Wanafunzi wote tisa waliosimamishwa shule wamerejeshwa shuleni bila masharti yoyote. Hatua za kiutawala na uongozi dhidi ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Izinga zitachukuliwa pindi uchunguzi unaoendelea utakapokamilika," alisema Hassan.

Kadhalika alisema serikali itahakikisha wanafunzi wa shule hiyo na nyingine katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi wanasoma bila kubughudhiwa wala kuingizwa katika migogoro yoyote ya kijamii na kisiasa.

Alisema baada ya kufanya mahojiano na wadau wakiwamo Ofisa Elimu Kata, Mtendaji Kata na Mwalimu Mkuu imebainika mwalimu mkuu aliwasimamisha wanafunzi hao tisa na kutaka wazazi wao wakatafute shule nyingine.

Alisema Wizara ya Elimu kupitia Mkuu wa Wilaya ya Nkasi haikuhusika kutoa maelekezo ya kusimamisha wa shule wanafunzi hao.

"Uamuzi wa kuwasimamisha wanafunzi hao haukutokana na itikadi za kisiasa za wazazi wa wanafunzi hao, bali ni mtafaruku uliojitokeza kati ya Mwalimu Mkuu, walimu na wazazi kutokana na kashfa, dharau na lugha chafu zilizotolewa na wazazi dhidi ya walimu wa shule hiyo kwamba, hawana sifa ya kufundisha watoto wao," alisema.

Hassan alisema uamuzi wa kuwasimamisha wanafunzi hao haukufuata utaratibu wa miongozo ya wizara, kwa sababu waliosimamishwa hawakuwa na kosa lolote la kinidhamu.

**BARUA**

Katika barua hizo zilizozagaa katika mitandao ya kijamii, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Izinga, Namanyere huko Nkasi, sehemu ya barua hizo inasomeka: "Rejea mada tajwa hapo juu. Walimu wote wa Shule ya Msingi Izinga, tumefikia maamuzi (uamuzi) ya (wa) kusimamisha shule watoto wako tajwa hapo juu (majina yamehifadhiwa) kutokana na kashfa na kauli mbaya ulizozitoa wewe mzazi siku ya tarehe 27/11/2024 wakati wa zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Kutokana na vitisho ulivyovitoa kwa walimu na dharau nyingi dhidi yetu, tumeona hatuna uwezo wa kufundisha watoto wako tena. Hivyo wewe kama mzazi wa watoto tajwa hapo juu, watafutie watoto wako shule yenye walimu unaowaamini kuwa ndio yenye uwezo wa kufundisha watoto wako."

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA



Aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Simba, Mwalami Sultan (wa pili kulia) na wenzake wakiongozwa na Askari Magereza, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusikiliza maelezo ya awali ya kesi inayowakabili ya kukutwa na dawa za kulevya aina ya Heroine zaidi kilo 34. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Toto Afya Kadi yarejeshwa, NHIF yanasa wadanganyifu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TOTO Afya Kadi inarejea. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umesema kuanzia Januari mwakani, watoto wenye umri usiozidi miaka 21 watanufaika nayo.

NHIF ilisitisha Toto Afya Kadi mwaka jana baada ya kubainika ilikuwa inasababisha hasara kubwa kwa mfuko kutokana na kundi hilo kutumia zaidi ya kile ilichokuwa inachangia kwa mfuko.

Vilevile, uongozi wa mfuko huo umesema umeokoa Sh. bilioni 5.44 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi 2024 kutokana na kuzuia mianya ya udanganyifu uliokuwa unafanywa na baadhi ya wanachama na vituo vya kutolea huduma za afya.

Akizungumza jana jijini Dodoma na wahariri wa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dk. Irene Isaka alisema wamefunga mifumo thabiti kudhibiti udanganyifu ambao ulifanywa na wanachama, watoa huduma na madaktari.

Dk. Isaka alisema mfuko huo unaelemewa na makundi matatu ambayo ni wenye umri mkubwa, wenye magonjwa yasiyoambukiza na Toto Afya Kadi.

Alisema kwa kipindi cha miaka saba kuanzia 2016/17 hadi 2023/24 cha huduma hiyo, walipata hasara ya asilimia 366 kulinganishwa na fedha ambazo wanufaika hao walichangia kwa mfuko.

Dk. Isaka alitolea mfano wa mwaka 2023 ambao wanufaika 185,021 walichangia Sh. bilioni 10.134 lakini walitibiwa na mfuko kwa gharama ya Sh. bilioni 31.764 sawa na hasara ya asilimia 313.

Mkurugenzi wa Huduma za Wanachama wa NHIF, Hipoliti Lelo, alisema mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote umeondoa sharti la kufikisha idadi ya wanafunzi 100 ndipo wasajiliwe kuwa wanachama na kupata huduma.

Lelo alisema kwa sasa shule au chuo kinaweza kusajili wanafunzi waliopo wasio na huduma hiyo na wakapewa huduma bila kujali idadi.

"Mfano, shule ina wanafunzi 80 halafu 20 wana bima, wale 60 waliobaki tutawasajili. Au wazazi wanasuasua kujiandikisha na tayari kuna wachache wako tayari, tutawasajili na wataendelea kuwa wanachama na kupata huduma," alisema.

Alisema utaratibu wa kuandikisha umeanza kwenye vyuo mbalimbali kwa wote wenye umri wa miaka 18 na kwamba wanaweza kujisajili moja kwa moja wenyewe.

**UDANGANYIFU**

NHIF imeokoa Sh. bilioni 5.44 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi 2025 kutokana na kuzuia mianya ya udanganyifu uliokuwa unafanywa na baadhi ya wanachama.

Dk. Isaka alisema wamekutana na matukio ya kadi ya mwanafunzi kutumiwa na watu watatu kujifungua ndani ya mwaka mmoja, na baada ya uchunguzi ilibainika aligawa kadi kwa watu wengine.

Pia wamebaini mwanachama kwenda kutibiwa malaria kisha kupewa vipimo na dawa nyingine ambazo hazihusiani na matibabu aliyoyapata.

"Tumekutana na matukio mtoto ameenda kufanyiwa tohara, lakini kalazwa kwa siku tatu, wakati ni huduma anayoipata kwa saa chache na kuondoka ila alilazwa kusubiri siku ya kutahiriwa kisha akafanyiwa na kupumzishwa siku ya tatu akaruhusiwa. Hii si sawa kwa kuwa ni huduma unayopata kwa saa chache na kuruhusiwa," alisema.

Alisema hatua zilizochukuliwa, kadi 12,685 zilifungiwa kutokana na udanganyifu, mikataba 11 ya watoa huduma imesitishwa na hivyo kufanya jumla ya mikataba 55 iliyositishwa tangu mwaka 2018.

Alisema watumishi watatu wa mfuko wamechukuliwa hatua za kinidhamu baada ya mashauri yao kukamilika na wengine wanane taratibu zinaendelea na hivyo kufanya jumla ya watumishi 11 waliochukuliwa hatua za kinidhamu.

Dk. Irene alisema watumishi wa sekta ya afya wapatao 36 taarifa zao zimewasilishwa katika mamlaka za kinidhamu.

**UHAI WA MFUKO**

Dk. Irene alisema uhai wa mfuko mwaka 2001/02 ulikuwa miaka saba na miezi tisa lakini ukashuka hadi miezi sita Juni mwaka jana, na ulipanda hadi mwaka mmoja Juni 2024.

Alisema makusanyo hadi Juni 2024 ni Sh. bilioni 756.48 sawa na asilimia 101.3 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 746.76.

Alisema asilimia 26.4 ya wananchi wanaishi chini ya mstari wa umaskini. Kati yao, asilimia 70 wako vijijini, wote wanastahili kupewa bima bila kuchangia.

Kwa mujibu wa Dk.Irene, kuna ongezeko kubwa la wazee wa kuanzia umri wa miaka 60 ambao wana changamoto kubwa za afya, hasa magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema vituo vya kutolea huduma za afya vyenye mkataba na NHIF na kiasi cha asilimia kwenye mabano ni serikali (73), sekta binafsi (18) taasisi za dini (9).

Alisema kwa kipindi cha kuishia Juni 2024 mfuko umelipa madai ya vituo vya kutolea huduma ya Sh.bilioni 650.4, ikiwa ni asilimia 37 vya serikali, 35 binafsi na 28 vya madhehebu ya dini.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***




# Mahakama yaelezwa kocha wa Simba alivyopokea dawa za kulevya, kuzitunza

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA imeelezwa aliyekuwa kocha wa makipa wa timu ya Simba, Muharami Sultani, alivyokuwa anapokea mzigo wa dawa za kulevya na kuutunza kutoka kwa mmiliki wa Kituo cha Michezo cha Cambianso, kilichoko Tuangoma, Kigamboni mkoani Dar es Salaam kupitia Bahari ya Hindi kutoka kwa raia wa Afghanistan.

Pia, imeelezwa mmiliki wa kituo hicho, Kambi Zuberi Seif, alivyokuwa kiongozi katika biashara ya dawa za kulevya aina ya heroin na kukamatwa katika mpaka wa Horohoro, Tanga akitaka kutorokea nchini Kenya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai hayo jana katika Mahakama ya hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, akisaidiana na Roida Mwakamele na Judith Kyamba wakati wakiwasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi baada ya upelelezi wa kesi ya usafirishaji wa kilogramu 34.89 za dawa za kulevya aina ya heroin inayowakabili kukamilika.

Mbali na Kambi na Sultani washtakiwa wengine ni Maulid Mzungu, maarufu kama Mbonde, Said Matwiko, Fundi Selemala, John Andrew maarufu kama Chipanda ambaye ni mfanyakazi wa Cambiasso na Sara Joseph ambaye ni mke wa Matwiko.

Wakili Mwanga alidai kuwa washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa mashtaka manane ambayo waliyatenda mwaka 2022 wakiwa ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam na eneo la Kamegele, Mkuranga mkoani Pwani. Akisoma maelezo hayo, Mwakamele alidai kuwa msiri aliwaeleza maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya (DCEA) kwamba Seif ameondoka nyumbani kwake, amepata taarifa kuwa Matwiko na Chipanda wamekamatwa.

Alidai kuwa taarifa hiyo ya msiri ilisababisha bosi wa mamlaka hiyo kuweka zuio katika viwanja vya ndege na kwenye mipaka ya nchi ili asitoke kwa sababu taarifa zilizokuwapo ni kwamba alikuwa anatorokea Kenya.

"Oktoba 30, 2022 majira ya usiku, maofisa wa DCEA waliweka mtego katika mpaka wa Horohoro mkoani Tanga ambako Seif alipanga kutoroka kwenda Kenya na alikamatwa akiwa katika harakati za kutoroka.

"Alikuwa na simu nne, hati ya kusafiria, Dola za Marekani 500 na Sh. 41,000. Oktoba 31, 2022 walimpeleka katika ofisi za DCEA, alipumzika kwa saa tatu na Novemba Mosi, 2022 alihojiwa na kukiri kumfahamu Chipe na washirika wake ni Ally Yusuph na Seleman," alidai Mwakamele.

Seif katika mahojiano hayo, alidai kuwa alipokea takribani pakiti 80 ya dawa za kulevya aina ya heroin kutoka kwa Yusuph ambaye alizipokea kutoka kwa raia wa Afghanistan ndiyo akampa yeye na yeye akampa Sultani azitunze.

Alidai kuwa aliendelea kumueleza ofisa wa DCEA kuwa biashara hiyo alianza mwaka 2019 kwa kuuza gramu moja kwa rejareja na kwamba dawa hizo alikuwa akizitoa kwa mtu aliyefahamika kwa jina la Hafidhi na Kevin Soko.

Pia alivyoulizwa kuhusu kama ana Kitambulisho cha taifa alidai hana na katika uchunguzi ilibainika kuwa anacho lakini laini zake za simu zimesajiliwa na kitambulisho cha mtu mwingine ili kuficha biashara hiyo.

Alidai kuwa alipopelekwa kwa mlinzi wa amani, yaani Mahakama ya Mwanzo Kigamboni, alikiri kuhusika na biashara ya kusafirisha dawa za kulevya.

Kabla ya maofisa hao kuweka mtego wa kumkamata, ilidaiwa kuwa walikwenda nyumbani kwake Oysterbay kwenye nyumba aliyopanga ya Mzee Kavishe kwa ajili ya upekuzi na walipofika walifunguliwa mlango na mdogo wake, Sabrina Seif, akadai kuwa kaka yake ametoka.

"Upekuzi ulifanyika nyumba nzima lakini chumba anacholala Kambi kilikuwa kimefungwa kwa sababu alikuwa na tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya. Kitasa cha mlango kilivunjwa na wakaingia ndani. Hawakukuta chochote bali Sh. milioni tisa ambazo zilichukuliwa," alidai.

Pia alidai kuwa katika uchunguzi, walibaini kuwa Kambi ni Mkurugenzi wa Kampuni Safia Group Company Ltd akiwa na hisa asilimia 60, Jamila Kambi asilimia 30 ambaye ni mke wake na kaka yake Ally Seif asilimia 10.

Katika uchunguzi maafisa hao, walibaini kuwa Kambi alikwenda kukopa magari matano aina ya Tata katika Kampuni Tata Motors kila gari alitanguliza Sh. milioni 30 na gharama ya magari yote ni Sh milioni 500. Ilidaiwa kuwa alifanya hivyo kuficha biashara yake ya dawa za kulevya.

Pia mahakama ilielezwa kwamba walipokwenda kufanya upekuzi nyumbani kwa Chitanda na Matwiko, walikuta na maboksi ndani yake kulikuwa vimfuko vilivyofungwa vikiwa na dawa za kulevya.

Katika kesi hiyo, washitakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 27, 2022 Kivule , Ilala mkoani Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kilogramu 27.10.

Katika shitaka la pili, ilidaiwa kwamba Novemba 4, 2022, eneo la Kamegele Mkuranga, kwa pamoja walikuwa wakisafirisha kilogramu 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroin.

# Askari mbaroni madai ya kuua raia kwa risasi

**Mussa Mwangoka,** MPANDA

ASKARI wawili wa Hifadhi ya Taifa ya Wanyamapori ya Katavi, wanashikiliwa na polisi mkoani Katavi kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga risasi kijana mmoja wa jamii ya kifugaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Kamishna msaidizi Mwandamizi (SACP) Kaster Ngonyani, alithibitisha kukamatwa kwa askari hao wanaodaiwa kufanya mauaji hayo Desemba Mosi, mwaka huu, katika kijiji cha Ikuba, Halmashauri ya Mpimbwe, wilayani Mlele.

Kijana aliyeuawa ni Ngimbangu Mandalu (25) ambaye anadaiwa kupigwa risasi na askari hao akiwa katika harakati za kuwakimbia pindi walipotaka kumkamata kwa madai ya kuingiza mifugo katika eneo lililohifadhiwa na kijiji ambalo shughuli za kibinadamu hiziruhusiwi kufanyika.

Baba mkubwa wa marehemu, Maduka Salawa, alisema siku ya tukio aliarifiwa kuwa mtoto wake amepigwa risasi, hivyo aliongozana na viongozi wa kata, akiwamo polisi na kufika eneo husika.

Alisema baada ya kufika ilibainika kwamba kijana huyo aliuawa akiwa nje ya mipaka ya maeneo hayo yanalindwa na askari wa TANAPA.

Salawa alisema baada ya askari hao kumpiga risasi kijana huyo, waliichukua maiti yake na kwenda kuitupa porini, lakini kutokana na ndugu wa marehemu kulalamika kwa viongozi wa juu wa wilaya na wa hifadhi, ndipo watuhumiwa walionesha maiti hiyo.

Kutokana na mazingira hayo, alisema ndugu wa marehemu waliamua kutochukua mwili huo hadi kupata tamko la serikali kuhusu mauaji hayo.

Alisema maiti hiyo ilikaa hospitalini kwa siku tatu ndipo jana walipoichukua na kwenda kuzika, baada ya kujiridhisha kwamba watuhumiwa wamekamatwa.

January Joseph, shuhuda wa tukio hilo, alidai watuhumiwa walimkimbiza Mandalu na baada ya kuona anawazidi mbio, walifyatua risasi na kumjeruhi mguuni upande wa goti, kifuani na begani.

## Uchaguzi mwenyekiti aliyepata kura nyingi za Hapana kurudiwa

**Na Vitus Audax**

MKOA wa Tabora umetangaza kurudiwa kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji katika wilaya ya Uyui, kijiji cha Ipululu na vitongoji viwili vya Stesheni na Nkene, baada ya mgombea mmoja kupigiwa kura nyingi za Hapana na wengine wawili kufariki dunia.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa huo, Elihuruma Nyerra, ilisema marudio ya uchaguzi huo yanatakiwa kufanyika ndani ya siku 40 baada ya uchaguzi.

Alisema mgombea huyo anatokea kata ya Loya, kijiji cha Magulyati, kitongoji cha Bukene na alikuwa mgombea pekee ambaye alipata kura nyingi za hapana, hivyo kuthibitisha kuwa hakuchaguliwa na wananchi, hivyo kulazimu uchaguzi huo kurudiwa.

"Wagombea wawili wakifariki dunia, mmoja ni wa kitongoji cha Stesheni kutoka chama cha ADC, aliyefariki dunia siku chache kabla ya uchaguzi, hivyo eneo hilo haukufanyika uchaguzi," alisema Nyerra.

Alisema mgombea mwingine aliyekuwa katika kundi mchanganyiko kijiji cha Ipululu, alifariki dunia wakati mchakato wa uchaguzi ukiendelea, hivyo kulazimu uchaguzi huo kurudiwa.

Nyerra alisema amemwelekeza msimamizi wa uchaguzi kuharakisha maandalizi ya marudio ya uchaguzi huo ili ufanyike ndani ya muda wa kikanuni.



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele, (kushoto) akikagua mafunzo ya watendaji wa uboreshaji ngazi ya jimbo yaliyofanyika kwa siku mbili katika kituo cha Shule ya Sekondari Ilboru, mkoani Arusha jana, ikiwa ni maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajia kuanza Desemba 11 hadi 17, 2024. **PICHA: INEC**

# Madaktari Tanzania wahudumia wagonjwa 2,770 kambi Comoro

**Na Joseph Mwenddapole**

MADAKTARI wa Tanzania wamerejea nchini baada ya kuhitimisha kambi tiba nchini Comoro kwa kutoa huduma kwa wagonjwa takriban 2,770 na kufanya upasuaji kwa wagonjwa saba.

Kwenye kambi hiyo ya siku saba, madaktari hao wamebaini wagonjwa takriban 269 wanahitaji rufani za matibabu zaidi nje ya nchi na pia kuainisha fursa zaidi za ushirikiano katika sekta ya afya.

Akizungumza jana baada kuwasili nchini, Mkurugenzi wa Global Medicare, ambao ndio waratibu wakuu wa kambi hiyo, Abdulmalik Mollel, alisema kambi imekwenda vizuri na wamefanikiwa kuwahudumia watu wengi.

Mollel alisema nje ya kambi hiyo walifanya kikao maalum na Waziri wa Ulinzi wa Comoro ambaye pia ni Msaidizi wa Rais na Katibu Mkuu wa Chama Tawala cha Comoro.

"Namshukuru Dk, Peter Kisenge (Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete- JKCI) kwa imani aliyoonyesha kunipa kazi ya kuandaa kambi. Naishukuru Wizara ya Afya kwa kunipa fursa ya kuandaa kambi hii, pia Prof. Mohamed Janabi (Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili- MNH) ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii Tiba.

Natoa wito hospitali kubwa nchini kufungua mipaka kwenda nchi jirani na sisi Global Medicare tutashirikiana kutimiza azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii tiba," alisema.

"Kwenye vikao kama saba tulivyofanya tulijadili fursa mbalimbali za uwekezaji na ushirikiano kwenye sekta ya afya baina ya Tanzania na Comoro na yeye Msaidizi wa Rais kwenye kikao aliongelea fursa kama watapatikana madaktari wa Tanzania kufanyakazi Comoro.

"Nje ya kambi tuliangalia uwezekano wa hospitali za Tanzania kuchukua kazi za hospitali moja ya Comoro yenye vitanda 100 na kuangalia uwezekano wa kuangalia utaalamu ambao haupatikani Comoro sisi Watanzania tuupeleke kwao," alisema.

"Tumefanya vikao mbalimbali vyenye tija, tumekaa na Waziri wa Afya wa Comoro na tumekaa na Mshauri Mkuu wa Rais wa Comoro kuangalia mambo ya msingi ambayo tunaweza kushirikiana na uwekezaji ambao umefanyika Tanzania," aliongeza.

Pia alisema walikaa na jumuiya inayojihusisha na elimu ya saratani Pamoja na Mkuu wa idara ya Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Comoro kuchambua kozi za afya ambazo wanazitoa kwenye vyuo vyao na ambazo hazitolewi kwao lakini Tanzania zipo ili kuzipeleka.

Mollel alisema vikao hivyo vilihudhuliwa na Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Said Yakub, Dk. Kisenge, Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Aisha Mahita na yeye mwenyewe.

Dk. Kisenge aliushukuru ubalozi wa Tanzania nchini Comoro na mratibu wa kambi hiyo, kwa kufanikisha kambi hiyo.

Aliishukuru wakurugenzi wenzake wa hospitali mbalimbali ambao waliridhia kutoa madaktari na wataalamu mbalimbali kwenda Comoro kushiriki kambi hiyo.

Alimshukuru Prof. Janabi, MOI, Ocean Road, Benjamin Mkapa, kwa kukubaliana kufanya kambi hiyo kwa pamoja na ambayo alisema imefanya kazi nzuri sana kuliko kambi iliyowahi kufanyika.

Dk. Kisenge alisema kambi iliyomalizika Comoro imekutanisha wadau mbalimbali na kufanya vikao vitakavyoleta tija kwenye ushirikiano wa sekta ya afya Comoro na Tanzania.

"Kwa uwekezaji tulio nao kwenye hospitali zetu ili nchi zinazotuzunguka zinufaike na uwekezaji huo lazima tumuunge mkono Rais wetu kwa kufanya kama Comoro na Global Medicare isichoke kuratibu kambi kama hizo kwa sababu tunataka kupiga hatua nyingine na madaktari wote nchini wawe tayari inapotokea kambi kama hii," alisema.

TOLEO MAALUM

# Ni rahisi sana kununua Hatifungani ya Samia Infrastructure Bond ya Benki ya CRDB

Wakati wa uzinduzi wa uuzaji wa Hatifungani ya Miundombinu ya Samia (Samia Infrastructure Bond - SIB) iliyotolewa na Benki ya CRDB, Rais Samia Suluhu Hassan alinunua hisa zenye thamani ya shilingi milioni 200.

Makamu wa Rais, Dkt. Phillip Mpango, ambaye alimwakilisha Rais Samia katika hafla hiyo, naye hakutaka kuachwa nyuma. Akanunua hisa zenye thamani ya shilingi milioni 100.

Watu waliohudhuria uzinduzi wa uuzaji wa hatifungani hiyo nao wakachangamkia fursa na kwa ujumla wao mpaka wakati sherehe za uzinduzi zinamalizika walikuwa wamenunua hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 37.

Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura), Benki ya CRDB imetoa hatifungani hii ili kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 150 zinatakazotunika kwenye miradi ya ujenzi wa barabara.

Kwa hatifungani hii ambayo ndio kwanza imezinduliwa kuuzwa, kuuza asilimia 25 ya thamani yake katika siku ya kwanza ni mafanikio ya aina yake. SIB, itakayodumu kwa kipindi cha miaka mitano, inalenga kutatua changamoto za kifedha katika ujenzi wa miundombinu nchini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, ingawa serikali imekuwa ikitenga rasilimali nyingi kwa ajili ya miradi ya miundombinu, ucheleweshaji wa malipo kwa makandarasi na changamoto za upatikanaji wa fedha zimesababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi mingi.

"Hatifungani hii inalenga kuhakikisha makandarasi wanaohusika na miradi ya barabara za mijini na vijijini wanalipwa kwa wakati, hivyo kuharakisha utekelezaji wa miradi," anasema Nsekela.

Hatifungani ya Samia Infrastucture Bond itakayodumu kwa miaka mitano inalenga kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 150. Fedha zitakazokusanywa zitapelekwa moja kwa moja kwa makandarasi ili kuhakikisha ujenzi wa barabara unaendelea kama ulivyopangwa.

"Hatifungani hii itahakikisha makandarasi wanapata fedha wanazohitaji, hivyo kuondoa ucheleweshaji na kuhakikisha miradi ya barabara inakamilika kwa wakati," anasema Nsekela.

Uuzaji wa hatifungani ya Samia Infrastructure Bond utakaodumu kwa siku 30 ulizinduliwa Novemba 29 mwaka huu na unatarajiwa kudumu hadi Januari 17 mwakani. Katika kipindi hiki chote, kila Mtanzania anayo fursa ya kununua moja kwa moja kutoka Benki ya CRDB na baada ya dirisha kufungwa itaorodheshwa katika soko la upili la Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE) kwa uuzaji na ununuzi wa baadaye.

## Unavyoweza kununua SIB

Watu watakaonunua hatifungani hii watakuwa wakishiriki moja kwa moja katika ujenzi wa miundombinu na wanaoweza kununua ni watu binafsi wakiwemo waajiriwa kutoka sekta ya umma na binafsi, Watanzania waishio nje ya nchi, wanafunzi, wastaafu na wawekezaji wa pamoja. Pia, vikundi kama vile vicoba, vikundi vya familia hata vikundi vya WhatsApp navyo vinaweza kununua hatifungani hii.

Kwa upande mwingine, taasisi za biashara, wajasiriamali wadogo na wa kati, taasisi za serikali na binafsi pamoja na mashirika nayo watakuwa na haki ya kununua hatifungani ya Samia Infrastructure Bond.

Hata hivyo, kuna mambo kadhaa ambayo mtu au taasisi inayotaka kununua hatifungani anapaswa kuyazingatia. Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Bonaventure Paul, mtu anahitaji kuwa na namba ya akaunti ya CDS ambayo inatolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pekee.

Hii ni akaunti maalum ambayo inatumika kwa ajili ya kununua, kuuza au kuhamisha hisa na dhamana kupitia masoko yanayofanya biashara hiyo. Na ni rahisi kuipata.

Baada ya kupata namba hiyo, mnunuzi anaweza kununua hatifungani hii kupitia Programu ya SimBanking, kwenda tawi lolote la Benki ya CRDB au kutumia mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

## Kununua kupitia SimBanking ya CRDB

Kabla hujaanza hatua yoyote ya ununuzi wa hatifungani, hakikisha unajielimisha mambo ya msingi kuhusu hatifungani husika ikiwamo kiwango cha chini unachoweza kununua, faida yake na muda wa uhai hatifungani yenyewe.

Mfano, hatifungani hii ya Samia, inalenga kukusanya shilingi bilioni 150 na itadumu kwa kipindi cha miaka mitano ikitoa faida ya asilimia 12 ya kiasi utakachonunua ambayo italipwa mara nne kwa mwaka.

Mwekezaji anaruhusiwa kuwekeza kiwango cha chini cha shilingi 500,000. Kwa uwekezaji huo wa shilingi 500,000, utampatia mwekezaji faida ya shilingi 300,000 ndani ya miaka mitano ya uhai wake. Na ukinunua hatifungani ya shilingi milioni 500, basi tarajia kuvuna shilingi milioni 800 hatifungani itakapoiva. Lakini siyo lazima usubiri miaka mitano kwani unaweza kupata gawio kila baada ya miezi minne.

Bonaventura anasema iwapo utanunua hatifungani kupitia SimBanking, utatakiwa kuingia kwenye simu yako na kwenda kwenye eneo la ununuzi wa Samia Infrastructure Bond. Hapa utakutana na maelekezo ya nini unatakiwa kufanya ikiwamo kujaza taarifa muhimu.

Zinazohitajika ni taarifa zako binafsi au za usajili wa taasisi kama ununuzi unafanywa na taasisi. Kisha utatakiwa kujaza namba yako ya CDS na pia taarifa zako za benki ili kuwezesha uhamishaji wa fedha kutoka kwenye akaunti yako kwa kiasi cha hatifungani utakachonunua.

Ukishakamilisha kujaza fomu zote kikamilifu, utatakiwa kuidhinisha malipo na app itakuletea taarifa za akaunti ambayo fedha zinapaswa kutoka na akaunti ambayo zitaingia.

Ukishaidhinisha malipo hayo na muamala kufanyika basi utapata risiti ya kuonyesha kuwa umefanya malipo. Risiti hii utaipata kwenye simu yako au kwenye barua pepe iwapo umeweka maagizo ya kupokea risiti kwa njia hiyo.


Kama ukiamua kuwatumia mawakala wa DSE basi ni rahisi pia. Unachotakiwa ni kuwa na vitambulisho vyako halali na namba ya CDS. Ukishafika kwa wakala atakusaidia ujazaji wa fomu na kufanya malipo na hapo utakuwa mmiliki halali wa hatifungani ya Samia Infrastructure Bond.

## Matawi ya benki ya CRDB

Jinsi mawakala wa soko la hisa watakavyokusaidia haina tofauti kabisa na




*Mgeni rasmi katika uzinduzi wa Samia Infrastructure Bond, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango akiwa kwenye hafla ya uzinduzi wa hatifungani hiyo inayokusudia kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 150 zitakazotumika kujenga barabara nchini.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango (katikati) akiwa ameshika mfano wa hati ya ununuzi wa Hatifungani ya Samia Infrastructure Bond. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.*

vile utakavyosaidiwa na maofisa wa Benki ya CRDB iwapo utaamua kwenda kwenye tawi la benki kununua hatifungani yako.

Cha msingi kuzingatia ni kwanza, uwe na taarifa za msingi kuhusiana na hatifungani husika, uwe na usajili wa CDS na uwe na vitambulisho vitakavyohitajika wakati wa ujazaji wa fomu.

Lakini, licha ya kuwa na vitu hivyo vyote inashauria kabla hujanunua hatifungani, pata ushauri kutoka kwa wataalamu wa masuala ya fedha ili wakueleze kinagaubaga faida za uwekezaji unaopanga kuufanya.

"Tumeweka njia hizi anuai za kununua hatifungani ili kuhakikisha tunamfikia kila Mtanzania mahali popote alipo, iwe ndani au nje ya nchi," anasema Bonaventura.

Ukishakamilisha ununuzi wa hatifungani, taarifa kuhusu hatifungani yako zitaonekana kwenye akaunti yako ya CDS baada ya siku chache.

Baada ya kukamilisha ununuzi hakikisha unaendelea kufuatilia taarifa kuhusu hatifungani nyingine zinazotolewa na Benki ya CRDB ili usipitwe na fursa ya uwekezaji zaidi pindi itakapojiri.

## Faida ya hatifungani ya SIB

Kuwekeza kwa kununua Samia Infrastructure Bond, kuna faida nyingi. Nsekela anasema mnunuzi atakuwa anashiriki moja kwa moja katika ujenzi wa miumbinu nchini kwani fedha zitakazokusanywa zitatumika kwenye miradi hiyo.

Pia, mwekezaji atajihakikishia uwekezaji salama na usalama wa fedha zake katika kipindi chote cha miaka mitano. Kwa mujibu wa wataalamu wa masuala ya uwekezaji, kuwekeza katika hatifungani ni moja ya njia salama na ya uhakika kwani si rahisi kupata hasara.

Ununuzi wa hatifungani ni uwekezaji pekee ambao mwekezaji anakuwa na uhakika wa kiwango cha faida atakachokipata pale anaponunua hatifungani hiyo. Mwekezaji pia atakuwa na uhakika wa malipo mara nne kwa mwaka yanayotokana na faida ya uwekezaji wake.

Lakini, wataalamu wanashauri kuwa iwapo mwekezaji ataweza, basi aiache faida yake ikusanyike pamoja ili hatifungani itakapoiva avune kitita kikubwa cha fedha.

Ifahamike pia kuwa uwekezaji huu hautozwi kodi, si kwenye kiwango kinachowekezwa au kwenye faida inayopatikana.

Lakini kununua hatifungani ya miaka mitano hakumaanishi kuwa utakuwa imezifungia fedha zako kwani unaweza kuuza hatifungani hiyo kupitia DSE au benki wakati wowote utakapohitaji au unaweza ukakopa benki kwa dhamana ya hatifungani hiyo na ukapata fedha ya kufanyia biashara, kutatua changamoto uliyonayo au kuwekeza tena.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi kufuta sherehe za serikali una manufaa makubwa

**KILA** mwaka nchini tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara) na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania, kumekuwa na maadhimisho katika matukio hayo makubwa na muhimu kwa nchi. Sherehe za Uhuru hufanyika Desemba 9 kila mwaka na zile za Muungano huadhimishwa Aprili 26 kulingana na tarehe za matukio hayo.

Katika kuadhimisha sherehe hizo, kumekuwa na shughuli mbalimbali yakiwamo magwaride yanayohusisha vikosi vya ulinzi na usalama kama vile Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania (JWTZ) likihusisha kamandi zake zote za nchi kavu, majini, na anga, Polisi na Magereza. Ili kufanikisha sherehe hizo, kunakuwa na maandalizi makubwa kama yakiwamo ya wanajeshi kufanya mazoezi kwa ajili ya magwaride hayo.

Maandalizi hadi maadhimisho hayo, hutumia fedha nyingi ambazo huhusisha posho kwa ajili ya maofisa wa majeshi na askari wanaojiandaa kwa gwaride la Uhuru au Muungano, hatua ambayo hugharimu mamilioni ya shilingi.

Kutokana na hali hiyo, kuanzia uongozi wa awamu ya tano chini ya Hayati Rais John Magufuli, sherehe hizo kwa baadhi ya miaka zimekuwa zikisimamishwa badala yake fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli hizo kutumika katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mwaka 2015 baada ya kuingia tu madarakani, kwa mfano, Magufuli alifuta sherehe hizo na badala yake akaagiza siku hiyo itumike kufanya usafi kwa kila mwananchi. Magufuli katika kauli yake alisema ni aibu kwa taifa kuadhimisha miaka 54 ya uhuru mwaka huo wakati taifa likikabiliwa na ugonjwa wa kipindupindu ambao kwa kiasi kikubwa unasababishwa na uchafu. Katika kuhakikisha usafi unafanyika, aliagiza watendaji wote wa halmashauri nchini kutayarisha vifaa vya usafi ili kila mwananchi ashiriki kikamilifu.

Aidha, mwaka 2016 Magufuli pia alifuta sherehe za Muungano na kuagiza zaidi ya Sh. bilioni mbili zilizokuwa zimeandaliwa kwa ajili ya kufanikisha hafla hiyo, zitumike kwa upanuzi wa Barabara ya Mwanza hadi Uwanja wa Ndege. Pia alifuta sherehe za Uhuru za mwaka huo na kuagiza zaidi ya Sh. bilioni tano zilizokuwa zimetengwa zitumike kupanua Barabara ya Morocco hadi Mwenge, Dar es Salaam.

Magufuli aliendelea na mfumo huo ambapo mwaka 2018 alitangaza sherehe za Uhuru kufutwa, hivyo kuagiza fedha zilizokuwa zimepangwa kufanikisha azma hiyo kutumika kwa ujenzi wa Hospitali ya Uhuru jijini Dodoma. Pia mwaka 2020, sherehe za Muungano zilifutwa na Sh. milioni 835.4 kutumika kununua vifaa vya hospitali hiyo.

Utamaduni huo wa kufuta maadhimisho ya matukio hayo makubwa kinchi, yameendelea hata wakati wa uongozi wa sasa wa nchi chini ya Rais Samia Suluhu Hassan. Juzi kwa mfano, Rais alitangaza kuwa sherehe za miaka 63 ya Uhuru zilizopangwa kufanyika Jumatatu ijayo zimefutwa na kuagiza fedha zilizotengwa kwa ajili ya hafla hiyo kuelekezwa katika kutoa huduma za kijamii.

Kufutwa kwa shehere hizo kumewaamsha Watanzania wengi kuwa kuna umuhimu kwa shughuli hizo kutokufanyika kwa matukio makubwa kama vile magwaride na shamrashamra ambazo huhusisha wanajeshi pamoja na halaiki na ngoma za makabila kutoka mikoa mbalimbali. Hali hiyo imedhihirisha kuwa kumekuwa na manufaa makubwa kiuchumi na kijamii kwa shughuli hizo kutokufanyika kwa mfumo wa maadhimisho.

Jambo la kujiuliza, kama sherehe hizo zisingefutwa hospitali ya Uhuru ingejengwa na baadhi ya vifaa vingepatikana? Barabara ya Mwanza hadi uwanja wa ndege mkoani humo ungejengwa. Kwa Dar es Salaam, barabara ya Morocco hadi Mwenge ingepanuliwa na kupunguza adha ya msongamano wa magari wakati wa asubuhi na jioni?

Kwa ujumla, kufutwa kwa baadhi ya sherehe hizo kumeonesha mafanikio makubwa kama ilivyoelezwa. Uamuzi wa viongozi hao unapaswa kupongezwa na uungwe mkono na Watanzania wapenda maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Vita vya utapiamlo vianzie ngazi familia mahali tuliko

**WADAU** wa Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto nchini, wamekuwa mstari wa mbele kuhamasisha jamii kushiriki katika mapambano ya kutokomeza udumavu wa watoto unaosababishwa na lishe duni.

Tatizo hilo la udumavu wa watoto, limeonekana kutikisa baadhi ya mikoa nchini, ikiwamo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya nafaka, matunda na mboga.

Chanzo kinaelezwa kuwa ni kutokana na wazazi na walezi hususan kinamama kuwa bize sana kwa kutumia muda mwingi kujishughulisha na shughuli za kiuchumi, kutokana na familia zao kukumbwa na umaskini wa kipato.

Inadaiwa kuwa, wanawake hao wamejikuta wakibeba jukumu la kuhakikisha familia zao zinakuwa na maisha bora, ambalo lilitakiwa kuwa ni la mwanaume ambaye ni baba wa familia.

Tafiti zimebaini kuwa kinamama hao baada ya kubeba jukumu hilo, wamejikuta muda mwingi wakitumia kufanya biashara na kukosa muda wa kulea watoto wao kwa kuhakikisha wanapata chakula bora cha kujenga afya.

Wataalamu hao wameenda mbali zaidi wakisema kuwa tafiti zao wanazofanya kila mara, zinaonyesha kuwa hali ya udumavu wa akili kwa watoto inazidi kuwa mbaya zaidi nchini kutokana na utapiamlo.

Wanasema, ili kukabiliana na tatizo hilo nchini kunahitaji ushirikishwaji na utoaji wa elimu ya mara kwa mara kwa wazazi na walezi kwa ajili ya kutambua namna ya kuboresha afya zao watoto.

**Wanasema, ili kukabiliana na tatizo hilo nchini kunahitaji ushirikishwaji na utoaji wa elimu ya mara kwa mara kwa wazazi na walezi kwa ajili ya kutambua namna ya kuboresha afya zao watoto.**

Ni aina ya vyakula wanavyotakiwa kuwapa na muda na kwani kutaimarisha miili yao kwa kupata lishe za aina yote.

Shime kinababa, shirikianeni na kina mama kupambana na hali hiyo ya udumavu wa akili kwa watoto kwa kuwa inaelezwa kuanza tangu ujauzito wa mtoto.

Kila mzazi anatakiwa kuelewa kuwa sehemu ya kumwandaa mtoto kuanzia miaka sifuri mpaka minane ili kukabiliana na udumavu wa akili.

Endapo kila mzazi atatenga muda wa kutosha kwa kumfanyika vitu vya kumchangamsha mtoto, kumtengenezea vifaa na zana za michezo zitamsaidia kuweza kumudu K tatu.

Kila mmoja wetu anafahamu hizo nguzo tatu; kusoma, kuandika na kuhesabu kabla ya kuanza kumpeleka shule kuanza masomo ya awali.

Utapiamlo kwa kiasi kikubwa, unatokana na wazazi kujenga mazoea ya kula vyakula fulani na kupuuza vyenye lishe.

Hiyo inatokana na baadhi kukaidi kufuata mlo kamili na kuwa ndicho chanzo kikuu cha tatizo hilo la utapiamlo, kwa watoto na udumavu wa akili.

Elimu kama hizo zimekuwa zikitolewa kliniki katika hospitali mbalimbali wakati mwanamke anapokuwa na ujauzito.

Wajawazito wanapohudhuria kliniki wanashauri aina ya vyakula vya kula ili kuhakikisha mtoto anayezaliwa anakuwa na afya bora na hiyo ndiyo elimu ya msingi inayotolewa.

Vyakula wanavyotakiwa kutumiwa ni pamoja na unga wenye virutubisho kwa ajili ya mtoto tangu anapokuwa tumboni hadi kuzaliwa.

Licha ya mapambano yanayofanywa na serikali kupitia wizara zake ikiwamo Ofisi ya Waziri Mkuu, kukabili tatizo hilo bado kuna haja ya mashirika yasiyo ya kiserikali kusaidia kutokomeza janga hilo kwa watoto.

Jamani! Katika kuhakikisha watoto wanakuwa na lishe bora na akili timamu tuige mifano muhimu kwa wengine kwani serikali haiwezi kufanya kila kitu.

Mbaya zaidi, wataalamu wa afya wamebaini kuwa 'wasichana' wanaong'ang'ania kufanyiwa upasuaji badala ya kujifungua kwa njia ya kawaida, nao wanachangia tatizo hilo kwa watoto wao.

# Wataalamu mipango miji wajifungia kuweka mikakati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU moja baada ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi kubaini wimbi la maeneo ya huduma za kijamii kubadilishwa matumizi, wataalamu wa mipangomiji wamejifungia kwa siku mbili jijini Dodoma kuweka mikakati namna ya kuhakikisha mipango iliyowekwa inadumu.

Akizungumza juzi kwenye Mkutano Mkuu wa Tisa wa Mwaka wa Maofisa Mipangomiji Tanzania, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji, Lucas Mwaisaka, alisema katika mkutano huo wataalamu hao wanajifanyia tathmini na kupata elimu namna ya kusimamia mipango wanayoipanga ili kuondokana na tatizo hilo.

"Tumejadili namna ya kutumia teknolojia kusimamia shughuli zote za mipangomiji, tumefanya kazi kubwa ya kuanzisha mfumo ambao umeunganishwa na e-ardhi ili kudhibiti na kufanya kazi kwa haraka kuwahudumia wananchi kupitia mifumo," alisema.

Alisema tangu bodi hiyo ianze kufanya kazi mwaka 2009 imesajili kampuni 101 na wataalamu 546 huku kampuni 11 na wataalamu 32 wamefutiwa usajili kutokana na kukiuka sheria ya mipango miji kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi (NLUPC), Joseph Mafuru, alisema upimaji na upangaji shirikishi wa moja kwa moja kwa wananchi kwenye mitaa na vijiji nchini ndio mwarobaini wa kuondokana na wimbi la ubadilishaji wa matumizi ya ardhi iliyopangwa.

Alisema kuna umuhimu kusimamia mipangomiji kuanzia kwa wananchi kwenye mitaa husika ili kuimarisha na kulinda maeneo hayo yasibadilishwe matumizi.

"Tumejifungia hapa wataalamu kuangalia njia gani tutumie kwenye 'development control' hili ni muhimu kwa sasa kama mtakumbuka kuna wakati Jiji la Dar es Salaam waliweka utaratibu wa kubandika kwenye mitaa ramani ya mipangomiji ambayo ilikuwa inaonesha maeneo ya makazi, biashara, viwanja vya michezo, maeneo ya kupumzikia, shule, hospitali na huduma zingine za msingi, hii inasaidia kuwafanya wananchi wa eneo husika kulinda maeneo hayo muhimu kwenye mitaa yao," alisema.

Katibu wa Chama cha Wataalamu wa Mipangomiji (TITA), Emanuel Luhamba, aliomba serikali kutoa kipaumbele kwenye sekta ya ardhi hususan kwenye mipangomiji kwa kuwa ni uumbaji mwingine wa pili baada ya Mungu.

"Kuna changamoto kubwa zinaikumba sekta ya mipangomiji ikiwamo uhaba wa rasilimali fedha ambazo zingewezesha kupima na kupanga miji yetu na vijiji kwa kuwa vijiji vya leo ndio miji ya kesho, fedha hizi wakati mwingine zinahitajika katika kutwaa maeneo ili yawe wazi uweke mipangomiji inayofaa," alisema.



Askari polisi wa mkoa wa kipolisi Ilala, Dar es Salaam, wanafunzi na wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, wakiwamo Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), wakishiriki maandamano ya kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, yaliyoanzia Shule ya Msingi Tabata na kushia eneo la Barakuda, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Biteko awataka waajiri kuzingatia utu

**Na James Kandoya**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewahimiza waajiri nchini kuongeza umakini na kuzingatia misingi ya utu mahali pa kazi ili iwe motisha na chachu kwa watumishi kuongeza ubunifu na ufanisi.

Dk. Biteko alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kwenye hafla ya utoaji Tuzo kwa Mwajiri Bora wa mwaka 2024.

Aidha, aliwapongeza waandaaji wa tuzo hizo na kuwataka kupanua wigo wa makundi ya ushiriki huku akisisitiza umuhimu wa utoaji wa motisha mahala pa kazi ili watumishi waongeze ari ya kufanya kazi kwa viwango na ubora wa juu.

"Mwajiri anachokihitaji kwa mwajiriwa ni muda na ujuzi wake basi. Hivyo, waajiri ongezeni umakini na utu mahali pa kazi na mkifanya hivyo, waajiriwa ambao wanatumia muda mwingi kazini, wataongeza ubunifu na ufanisi na kuleta tija ya kazi," alisema Dk. Biteko.

**Alisema kuwa serikali inatambua mchango wa Chama cha Waajiri (ATE) nchini katika maendeleo na programu mbalimbali za maendeleo ikiwamo suala la ukuzaji wa uwiano wa kijinsia mahali pa kazi.**

Alisema kuwa serikali inatambua mchango wa Chama cha Waajiri (ATE) nchini katika maendeleo na programu mbalimbali za maendeleo ikiwamo suala la ukuzaji wa uwiano wa kijinsia mahali pa kazi.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Ridhiwan Kikwete, alisema serikali kwa kushirikiana na ATE na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini TUCTA imeongeza makundi ya ushiriki kwa waajiri, ikiwamo kigezo cha utambuzi wa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi pamoja na mwajiri anayezingatia masuala ya usawa wa kijinsia katika uajiri.

Alisema kuwa kwa msingi huo, Tanzania inajitanabaisha kimataifa kwa kuwa na kiongozi mkuu mwanamke (Rais Samia Suluhu Hassan), suala ambalo amesema linaiweka nchi katika nafasi ya juu kimataifa katika masuala ya usawa wa kijinsia.

Naye Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzan Ndomba-Doran, alisema kuwa tangu kuasisiwa kwa tuzo za mwajiri bora wa mwaka takribani miaka 19 iliyopita washiriki wamekuwa wakiongezeka na kuongeza ufanisi na waajiri kuboresha mazingira ya kazi.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Kanda ya Afrika Mashariki, Caroline Mugalla, alipongeza hatua iliyofikiwa katika utoaji wa tuzo hizo na alishauri mashindano hayo pia yahusishe na kutambua shughuli za vijana katika sekta isiyo rasmi ambayo ina mchango mkubwa katika jamii.

"Ni muhimu kuangalia namna ya kutambua mchango wa sekta isiyo rasmi ili kuweza kupata ajira zenye staha," alisema Mugalla.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# REA kutoa mitungi ya gesi 19,000 kwa ruzuku

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIKA kuziwezesha kaya za vijijini na mijini kutumia nishati safi ya kupikia serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), itatoa mitungi ya gesi 19,530 yenye ruzuku kwa Mkoa wa Singida ambayo itauzwa kwa bei ya chini ya Sh. 20,000 kwa mtungi mmoja.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, akizungumza juzi baada ya kupokea maofisa kutoka REA ambao wameleta mradi wa usambazaji wa mitungi ya gesi yenye ruzuku, alisema mitungi hiyo itagawiwa kwa uwiano sawa katika wilaya zote tano za mkoa huo ili kuhakikisha wananchi wananufaika.

Alisema ujio wa mradi huo ni faraja kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida kutokana na kwamba ni asilimia 20 tu ndio wanaotumia nishati safi ya kupikia kiwango ambacho ni kidogo sana ukilinganisha na kaya zilizopo mkoa hapa.

"Mkoa wa Singida tulishaanza kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi kupikia, kwa hiyo hili ambalo REA mmetuletea ni habari njema sana hasa ikizingatia kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakiomba bei ya mitungi ya gesi ipunguzwe, nampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuja na suluhisho," alisema.

Naye Mhandisi Mwandamizi kutoka REA, Deusdedit Malulu, alisema mradi wa kusambaza mitungi ya gesi yenye ruzuku kwa Mkoa wa Singida itaanza kutekelezwa Januari 2025 ambayo itakuwa na ujazo wa kilo sita.

Alisema mradi huo ambao unatekelezwa kwa nchi nzima jumla ya mitungi 452,000 itasambazwa katika mikoa yote nchini na itauzwa kwa bei ya ruzuku Sh. 20,000 badala ya Sh. 40,000 hadi 45,000.

Malulu alisema katika Mkoa wa Singida kila wilaya itapewa majiko 3,255 na idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na kaya zilizopo mkoa huu na kwamba huo ni mradi wa majaribio kutakuwa na mingine ambayo itatengewa fedha kwa mwaka wa fedha ujao.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwataka wananchi kuondokana na matumizi ya nishati chafu ambayo imekuwa na madhara kiafya na mazingira na vigezo vitakavyotumika kupata mitungi ya gesi ya ruzuku ni kuwa na kitambulisho cha NIDA.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza matumizi ya nishati safi kutokana na madhara yaliyopo upande wa afya na mazingira, nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi wa Mkoa wa Singida kuchangamkia fursa hii ya mitungi ya gesi yenye ruzuku," alisema.

Malulu alisema wananchi wabadilike na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia kwa kuwa serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa ajili ya kutibu magonjwa yanayosababishwa na kutumia nishati chafu.



Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Masozi Nyirenda (kushoto), akikagua mradi wa maabara ya sayansi katika Shule ya Sekondari Nyakitonto, mkoani Kigoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Milioni 180/- zakarabati shule Kigoma

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

ZAIDI ya Sh. milioni 180.7 zimetumika kufadhili ujenzi na ukarabati wa maabara za Sayansi, vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika shule mbili za Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma.

Ufadhili huo umetokana na ushirikiano kati ya Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) na Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Shule ya Sekondari Nyakitonto, imenufaika na ukarabati na umaliziaji wa maabara tatu za Sayansi (Kemia, Fizikia na Biolojia) kwa gharama ya Sh. milioni 60.1.

Mkuu wa shule hiyo, Akwilino Kidava, alisema ilikuwa na maabara moja hapo awali, lakini sasa wanafunzi watapata fursa ya kujifunza kwa vitendo, hatua inayotarajiwa kuongeza udahili na ubora wa masomo ya sayansi.

Shule ya Msingi Mkuyuni, imenufaika na ukarabati wa vyumba vinne vya madarasa pamoja na ujenzi wa matundu 12 ya vyoo kwa gharama ya Sh. milioni 120.5.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, Ombeni Mbembati, alisema kuwa shule hiyo yenye wanafunzi 1,057 ilikumbwa na tatizo la uhaba wa madarasa na matundu ya vyoo, hali iliyolazimu wanafunzi kusoma kwa awamu.

Iyogo Isuja ambaye ni Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, alitoa shukrani kwa UNICEF na TEA kwa uwekezaji huo ambao utaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Mwanafunzi wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Nyakitonto, Alex Malingumu, alisema maabara hizo zitawawezesha kufanya vizuri katika masomo ya sayansi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Nyakitonto, Adam Charles Ligula, alisema maabara za sayansi zitakuwa chachu ya kuhamasisha wanafunzi kusoma masomo hayo.

Miradi mingine 13 yenye thamani ya Sh. milioni 834.3 imefadhiliwa katika mikoa ya Tabora, Kigoma na Songwe.

Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa maabara, vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari, hatua inayolenga kuboresha elimu.

# Waziri Mkuu asisitiza umuhimu utoaji haki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema mfumo wa utoaji haki ni muhimu kwa ustawi wa utawala wa sheria, utawala bora na uhuru wa mahakama kwa kuwa vinachangia ukuaji wa uchumi.

Alisema hayo juzi jijini Arusha, wakati akifungua mkutano mkuu wa 21 wa Chama cha Mahakimu na Majaji wa Afrika Mashariki (EAMJA) kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Majaliwa alisema mfumo wa utoaji haki ni muhimu kwa ustawi wa utawala wa sheria, utawala bora na uhuru wa mahakama, kwa kuwa ni muhimu katika ukuaji wa uchumi.

Akinukuu kaulimbiu ya mkutano huo: 'Kuimarisha Mfumo wa Utoaji Haki kwa Mtangamano wa Kikanda na Ukuaji wa Uchumi,' alisema kuwa inalenga kukuza mfumo wa utoaji haki, ushirikiano wa kikanda na ukuaji wa uchumi.

"Mfumo ulioimarishwa wa utoaji haki wa mahakama ni muhimu kwa utangamano wa kikanda na ukuaji wa uchumi, mkutano huu unaowaleta pamoja Mahakimu na Majaji wa Afrika Mashariki ili kushughulikia masuala muhimu ya kitaifa na kikanda, unawapa fursa ya kujadili changamoto zinazotukabili katika utoaji haki na kuweka mikakati ya kukabiliana nazo," alisema Majaliwa.

"Mfumo wa utoaji haki ni muhimu kwa kuzingatia utawala wa sheria, utawala bora na uhuru wa mahakama, hivyo, EAMJA kinatuwezesha kushirikiana katika upatikanaji wa haki kwa wananchi wetu."

Pia, alibainisha kuwa uwekezaji wa teknolojia za kisasa na bunifu mbalimbali katika michakato ya mahakama ni muhimu katika kufikia utoaji wa haki wenye tija na ufanisi.

Majaliwa aliwataka kuzingatia jambo hilo kwa kuwa uwekezaji katika teknolojia unaweza kuleta mapinduzi katika mifumo ya usimamizi wa kesi, kuimarisha upatikanaji wa haki, na kufanya utoaji wa huduma za kisheria kuwa na ufanisi zaidi.

Alisisitiza kuwa mfumo bora wa teknolojia si tu unapunguza gharama, lakini pia unaokoa muda na rasilimali, kufikisha huduma za mahakama karibu na wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Nchi nyingi ulimwenguni zinaunda upya mifumo yao ya haki na utawala kwa kukumbatia teknolojia za kisasa, ikiwa ni pamoja na akili mnemba (AI), hivyo tujiandae kukumbatia mabadiliko haya," alisisitiza.

Akizungumzia mageuzi ya Mahakama ya Tanzania, Majaliwa alisema chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imefanya mageuzi muhimu ya kisera kijamii na kiuchumi ambayo yanachagiza mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa lengo la kuboresha ustawi wa wananchi.

Kwa mujibu wa Majaliwa, sera hizo, pamoja na mambo mengine, zinalenga kuimarisha uwezo wa kitaasisi ndani ya mfumo wa utoaji haki ili kukuza haki za kimsingi za mtu binafsi, kuongeza mchango wa mahakama katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuboresha utumiaji wa teknolojia za kisasa zinazosaidia kuwa na mahakama inayozingatia raia.

Pia, aliwataka wajadili uhalifu wa kimataifa wa kupangwa ambao ni tishio kwa usalama wa kitaifa, kikanda na kimataifa.



## HABARI KASKAZINI

# Mabilioni kuchanja mifugo nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 23 kwa ajili ya kampeni ya kutoa chanjo za mifugo kitaifa na kuwezesha wafugaji kufuga kwa tija.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kongamano la kisayansi la 42 la Chama cha Madaktari wa Wanyama Tanzania.

Ulega, alisema kampeni hiyo itafanyika kuwa kuwa ndio njia pakee ya kutokomeza magonjwa ya mifugo nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha Kitaaluma cha Wanyama Tanzania (TVA), Profesa Esron Karimuribo, alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali imetenga Sh. bilioni 460 kwa Wizara ya Mifugo na Sh. bilioni 28.1 kutoa chanjo kwa mifugo.

Karimuribo, alisema TVA imekuwa ikiendesha mikutano yake kwa mwaka kwa madaktari wa mikoa mbalimbali kwa ajili ya kubadilisha uzoefu na namna kukuza sekta ya mifugo nchini.

Prof. Esron, alisema pamoja na mambo mengine wamepata mafanikio makubwa katika sekta hiyo.

Aliyataja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni mauzo ya mifugo na mazao yake nje ya nchi na kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Alisema mafanikio mengine ni kudhibiti magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na kukuza uchumi wa wafugaji na wavuvi.

**Aliyataja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni mauzo ya mifugo na mazao yake nje ya nchi na kuliingizia taifa fedha za kigeni.**

Hata hivyo, alisema bado wanakumbana na changamoto ikiwamo kufikia malengo waliyojiwekea, upungufu wa madaktari wa mifugo wapatao 258.

Aliiomba serikali kutoa ajira kwa madaktari wengine wa mifugo ili kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuendana na kasi yake.

Baadhi ya wadau wa mifugo walioshiriki kongamano hilo, walishukuru serikali kwa kutokomeza magonjwa ya mifugo nchini.

Salim Msellem, ni mmoja kati ya wadhamini wa kongamano hilo, alisema kama wamiliki wa viwanda vinavyozalisha dawa na pembejeo za mifugo, alisema mifugo kwa kiwango kikubwa inasaidia kuinua pato la nchi.

"Tumefurahia kampeni ya chanjo kutolewa bure kwa mifugo, kwani ni jambo ambalo halijawahi kutokea kwa miaka mingi," alisema Msellemen.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha nia ya kusaidia viwanda vya kuzalisha dawa na pembejeo za kilimo nchini na kumshukuru kwa kupunguza tozo.

Aliiomba serikali kuendelea kushirikiana na sekta binafsi kukuza sekta ya mifugo na uvuvi.



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert (kushoto), akigawa miche ya miti kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kazima, mjini Tabora mapema wiki hii, kwa ajili ya kuipanda shuleni hapo, ili kuboresha mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii waongezeka Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

IDADI ya watalii wa ndani wanaotembelea vivutio eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imeongezeka hadi kufikia 200,000 katika kipindi cha miezi minne iliyopita.

Akitangaza kuanza rasmi kwa kampeni maalum ya kuchochea ongezeko la watalii wa ndani nchini maarufu kama Merry & Wild, Ngorongoro Awaits, Meneja Idara ya Utalii na Masoko wa NCAA, Mariam Kobelo, alisema watalii hao walitembelea vivutio hivyo katika kipindi hicho cha kati ya Julai na Novemba mwaka huu.

Kabelo, alisema hatua hiyo imekuja kutokana na mamlaka hiyo kutangaza vivutio hivyo ndani na nje ya nchi.

Akizungumzia kuhusu kampeni hiyo, alisema itawawezesha Watanzania wengi kutembelea vivutio hivyo vilivyopo Ngorongoro.

"Mamlaka ya Ngorongoro tumeamua kuanzisha kampeni hii kwa mwaka huu ili kuwawezesha Watanzania wengi kutembelea maeneo ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kujionea uzuri wa vivutio vilivyopo.

Aliyataja maeneo yenye vivutio kama urithi wa utamaduni wa Olduvai, Kreta ya Empakai, Olmoti na mlima wa tatu kwa urefu Tanzania wa Loromalasi.

Mengine ni Makumbusho ya Jiolojia ya Ngorongoro maarufu kama Ngorongoro-Lengai UNESCO Geopark.

Kobelo, alisema kifurushi cha kwanza kinachoitwa faru, kitamgharimu Mtanzania Sh. 450,000 kwa kufanya utalii kwa siku mbili ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sikukuu ya Krismasi, kati ya Desemba 24 na 25, mwaka huu.

Kifurushi cha pili tembo, chenye gharama ya Sh. 130,000 kwa mtu, kinahusisha utalii kwa siku moja. Wakati cha tatu ni chui chenye gharama ya Sh. 85,000 kwa mtu. Katika utekelezaji wa kampeni hiyo, NCAA inatarajia kutumia vikundi vya sanaa vikiongozwa na vijana ambao watakuwa katika mitaa ya mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Zanzibar kuanzia Desemba 4 hadi 16, mwaka huu.

# SADC, EAC wajadili miradi ya umeme Afrika

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NCHI za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Jangwa la Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimetakiwa kuainisha mikakati ya kitaifa na kikanda kutekeleza miradi mikubwa ya umeme itakayodumu kwa muda mrefu.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alitoa wito huo jijini hapa wakati akifungua Mkutano wa Kikanda wa Masuala ya Matumizi Bora ya Nishati wenye Kauli Mbiu ya Mkutano ni "Kuchagiza Matumizi Bora ya Nishati kwa Maendeleo Endelevu."

Biteko, alisema endapo SADC na EAC zikiainisha mikakati hiyo na kupata usaidizi wa kifedha kutekeleza miradi mikubwa watapata nishati ya kuaminika, kupunguza uzalishaji wa gesi chafu na kukuza uchumi.

Alisema takwimu zinaonesha ufanisi wa nishati duniani umeimarika kwa asilimia 1.1 kwa mwaka 2023 chini ya lengo lililokusudiwa.

"Kila nchi ni vema zikafuata njia mahususi katika kutekeleza sera, mikakati na teknolojia inayotoa fursa ya kipekee ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda kwa kujifunza kutoka kwa changamoto na mafanikio," alisisitiza Biteko.

Aliendeleza kuzitaka jumuiya hizo kuwekeza katika utafiti na maendeleo, kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa ndani na kuhakikisha teknolojia za ufanisi wa nishati zinapatikana na kununuliwa kwa mahitaji ya kipekee ya jumuiya hizo.

Amon Manyama kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), alisisitiza wataalamu kuweka mikakati ya matumizi ya nishati ili kuwa na kauli moja za kikanda kwa nchi za SADC na EAC na kuhakikisha Bara la Afrika linakuwa la kijani.

"Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita UNDP imefanya kazi na Wizara ya Nishati na wadau wengine kutekeleza Mpango Kazi wa Ufanisi wa Nishati unaowiana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia (WB) nchini ambaye anawakilisha Malawi, Zambia, Tanzania na Zimbabwe, Nathan Belite, alisema

maeneo ambayo shughuli za kiuchumi zinakua, upatikanaji wa umeme wa uhakika ni mdogo.

Belite, alizipongeza jumuiya hizo kwa kuandaa mkutano huo wa kikanda wa matumizi bora ya nishati.

"Benki ya Dunia inajivunia ushirikiano na serikali za nchi za Afrika katika bara zima ambapo miradi ya ushirikiano inakua ikiwamo mpango mkakati wa miaka 10 wa matumizi sahihi ya nishati," alisema.


Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk. David Mathayo, alisema nishati bora ni msingi wa mabadiliko ya uchumi na mazingira.

Mathayo, alisema ni vema kuendeleza viwango vya kikanda na kuweka mitandao ya nishati iliyounganishwa mipakani na kuleta ufanisi katika mifumo.

Alisema mifumo yenye nishati bora huboresha nishati bora na kupunguza utegemezi wa mafuta na utoaji kaboni ili kutimiza mkataba wa nishati.

"Tuzifanye nchi za Afrika Mashariki kuwa na matumizi sahihi ya nishati bora na sera za nishati bora zinaendelezwa," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, alisema kunahitaji kuangalia nishati hiyo kwa uangalifu na ubora.





# M'kiti Chadema avamiwa, ashambuliwa

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Muyaga C (CHADEMA) kilichopo Kata ya Kitahana, Onesmo Mdollo (40), anadaiwa kushambuliwa na watu wasiojulikana baada ya kumvamia wakati akitoka kazini.

Mdollo ambaye pia askari wa Kampuni ya Kiwango Security anadaiwa kukumbwa na mkasa huo mapema wiki hii asubuhi wakati akitoka katika kazi yake ya ulinzi Kanisa Katoliki la Kibondo akielekea nyumbani kwake.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa CHADEMA wa Wilaya ya Kibondo, Anselmo Matabalo, alisema: "Alikuwa (Mdollo) katika pikipiki yake ndipo alipovamiwa na watu wasiojulikana ambao walimpiga sehemu mbalimbali za mwili, wakachukua baadhi ya vitu vyake, ikiwemo pikipiki kisha wakamtupa pembeni ya barabara karibu na Kabwigwa,"

**Matabano, alisema Mdollo, amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo kutokana na hali yake kuwa mbaya baada ya kushambuliwa na watu wasiojulikana na kutupwa barabarani.**

Matabano, alisema Mdollo, amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo kutokana na hali yake kuwa mbaya baada ya kushambuliwa na watu wasiojulikana na kutupwa barabarani.

Kwa mujibu wa Matabalo, hali ya afya ya mwenyekiti huyo ni mbaya kwa kuwa mpaka sasa hana fahamu.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Phillemon Makungu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwa jeshi la hilo linafanya uchunguzi ili kubaini chanzo chake na kuwasaka watu waliohusika.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Cornely Nikibi, alithibitisha kumpokea Mdollo hospitalini hapo na kumfanyia uchunguzi na kubainika ameumia sehemu za kichwani.




Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Kitengo cha Dawati la Jinsia Wilaya ya kipolisi Msalala, mkoani Shinyanga, Joseph Kazurunga, akizungumza na wanafunzi wa kike kutoka wilaya hiyo mapema wiki hii, wakati wa kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Marufuku kuwaficha watoto wenye ulemavu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wamepigwa marufuku kuwafungia ndani watoto wenye ulemavu kutokana na imani za kishirikina na kuwapeleka shule kupata elimu na kutimiza ndoto za kuwa na maisha bora.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Elimu Kata wa Uyogo, Hassan Mwale wakati akizungumza na wakulima wa Chama cha Msingi Uyogo na Mshikamano.

Akizungumza katika mikutano mikuu ya vyama hivyo kujadili mapato na matumizi, upatikanaji wa mbolea na viwatilifu na kuongeza uzalishaji wa tumbaku na pamba, Mwale, alisema ametoa amri hiyo baada ya kubaini kuna baadhi ya familia za wakulima zenye watoto wenye ulemavu wamekuwa na tabia ya kuwaficha kwa kuwafungia majumbani na kutowapeleka shule kutokana na imani za ushirikina kuwa na mtoto wa namna hiyo ni mkosi na kusababisha kukosa haki ya msingi ya kupata elimu.

Mwale, alisema wamekuwa wakipitia kila kijiji kufanya mikutano ya hadhara ili kukemea vitendo hivyo. Alisema wakati mwingine wamekuwa wakipata taarifa kutoka kwa wananchi kuhusiana na familia yenye mtoto mwenye ulemavu na kwenda kutoa elimu na kumwandikisha kuanza masomo.

"Shule yetu ya msingi Bukwimba inapokea wanafunzi wa namna hii na wana walimu wao mahususi kuhakikisha wanatimiza malengo ya kielimu, mpaka sasa tuna jumla ya wanafunzi 13, wanane wa kike na watano wa kiume na wote wanahudumiwa na serikali kila kitu," alisema Mwale. Alisema walikuwa wakiwaibua watoto hao kwenye familia za wakulima kwa kushirikiana na wenyeviti wa vijiji na vitongoji.

Aliwataka viongozi waliochaguliwa hivi karibuni katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji kuendelea kutoa ushirikiano ili kila mtoto mwenye ulemavu apate haki yake ya msingi ya elimu.

Mwalimu wa Makundi Maalumu wa Shule ya Msingi Bukwimba, Joseph Nestory, alisema wanapokea wanafunzi wenye ulemavu na kutumia utaalamu wa namna ya kuwafundisha na kuhakikisha kila mmoja anasoma, kuipenda shule na kutimiza ndoto zao.

Mkulima wa tumbaku na pamba, Richard Mushi, alisema baadhi yao wanawaficha watoto wenye ulemavu kwa kuwafungia ndani kwa kuogopa kuchekwa na majirani.

Aliiomba serikali kuwachukulia hatua kali wazazi na walezi watakaobainika kuwaficha watoto ili wachukuliwe hatua za kisheria na kuwa fundisho kwa wengine.

# Mke adaiwa kuchoma moto nyumba ya mumewe

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKAZI wa Mtaa wa Mgusu Halmashauri ya Mji wa Geita, Michael Nzumbi hana makazi baada ya nyumba yake kuchomwa moto na anayedaiwa kuwa mkewe kutokana na mgogoro wa kifamilia.

Tukio hilo lilitokea Jumapili iliyopita majira ya asubuhi wakati mwanaume huyo akiwa kwenye ibada kanisani.

Inadaiwa kuwa Michael akiwa kanisani, alipigiwa simu na kupewa taarifa kuwa nyumba yake inatetekea kwa moto.

Michael, alisema baada ya kufika nyumbani kwake, aliwakuta majirani na wananchi wengine, wakiendelea kuzima moto huo.

Alisema jitihada za kuzima moto huo ziligonga mwamba kwa kuwa ulikuwa pia umeteketeza samani, vyakula, mavazi na fedha taslimu zaidi ya Sh.200,000.

Alidai jirani zake ndio waliomtambua mkewe huyo kuwa ndiye aliyechoma nyumba hiyo.

Michael, ameiomba serikali kuingilia kati kwa kumchukulia hatua kali kwa mkewe huyo kutokana na kitendo hicho alichodai kuwa ni cha kikatili dhidi yake.

Alidai mkewe huyo amekwisha kufanya majaribio kadhaa ya kumdhuru kwa nyakati tofauti, ikiwemo kumuunguza kwa kumwagia maji ya moto na kuchoma nyumba hiyo.

"Mgogoro wangu na mwanamke huyo ulianza muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja akinituhumu kuchepuka," alidai Michael na kuongeza kuwa:

" Baada ya kuchoma hati ya ndoa na kunimwagia maji ya moto niliamua kumuachia nyumba iliyopo mjini Geita, lakini amekuja tena kuchoma nyumba yangu."

Baadhi ya mashuhuda, walisema baada ya kufika katika eneo hilo, walikuta nyumba hiyo ikiwaka moto na kulazimika kuvunja mlango na kuanza kuzima kwa kumwagia maji na mchanga.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mgusu, Emmanuel Mapalala, alisema baada ya kufika eneo la tukio, alikuta nyumba hiyo ikiwaka moto na kushirikiana na wananchi kuuzima.

"Kabla ya tukio hilo, kulikuwa na mgogoro wa muda mrefu wa kifamilia kati ya wanandoa hao, lakini kama kweli mkewe amefanya tukio hili basi serikali ichukue hatua kwani kama angekutwa ndani mwanaume huyo angekufa," alisema.

Alifafanua kuwa baada ya kufika katika eneo hilo, waliomba msaada kwa mafundi wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) kuzima mfumo wa umeme ili kuruhusu wananchi kuendelea kuzima moto huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kutaja chanzo chake kuwa ni mgogoro wa kifamilia.

Kamanda Jongo, alisema jeshi hilo linamsaka mtuhumiwa huyo kwa tuhuma za kuchoma moto nyumba ya mumewe na kwamba akikamatwa atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka.



Ukurasa 12

Namna gani unaifahamu biashara ya kuasili, inavyomudu ushindani na hatari ya hasara?

**BUFE**

IJUMAA DESEMBA 6, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

MAISHA MAPYA WAKULIMA 100...

## Mradi pampu maji ya umeme wawapatia walima mboga mtoni Kisarawe na Rufiji

SAMIA NA SAFARI ZA KUTETEA SIKU YA UHURU...

# Alianza akikaribisha makomredi EAC, akahamia SDG za UN kunadi Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alitangaza kusitisha Sherehe za Uhuru mwaka huu.

Huo sio uamuzi mpya, kwani hata Rais mtangulizi wake, Dk. Samia akiwa Makamu wa Rais alifanya uamuzi kama huo, fedha husika zikawekezwa kwenye mradi wa barabara ya Morocco hadi Mwenge, Dar es Salaam.

Ikirejewa, siku aliyoendesha Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa mara ya kwanza madarakani, zilizofanyika Desemba 9, 2021 katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, mgeni rasmi alikuwa jirani yake walioasisi Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais Uhuru Kenyatta.

Pia, kukawapo ugeni wa marais; Paul Kagame (Rwanda), Philepe Nyusi (Msumbiji), Azali Assoumani (Visiwa vya Comoro), pia wawakilishi wa viongozi kutoka nchi za Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Burundi, Oman na Uswatini, pia mabalozi wa kigeni walioko nchini.

Ni tukio ambalo Rais Samia akakagua gwaride lililoandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kushirikiana na majeshi mengine ya ulinzi na usalama nchini.

Hilo likaendana na Rais kutunuku nishani 14, kwa watendaji 893 wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini.



Rais Samia Suluhu Hassan, akihojiwa jambo na mfanyakazi wa Umoja wa Mataifa, kuhusu lugha ya Kiswahili, alipokuwa ziarani huko, mwaka 2021. **PICHA: MTANDAO**

**ANADI VYAKE UN**

Ikiwa ni wastani wa miezi saba baadaye, mnamo Julai 7, 2022, Ubalozi wa Kudumu wa Tanzania nchini Marekani kwa kushrikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) zikaandaa maadhimisho makubwa ya Siku ya Kiswahili.

Ni tukio lililoibua tena sauti ya Rais Dk.Samia, akipongeza kwa ufafanuzi kwamba, "lugha hiyo ni alama ya Uhuru, Amani na Umoja."

Akihutubia wahudhuriaji wa maadhimisho katika makao makuu ya Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani Dk. Samia kwa njia ya video, akafafanua: "Msishangae kwanini nimeihusisha siku hii na Uhuru, Amani na Umoja.

"Nimefanya hivyo, kwa sababu Kiswahili kilitumika kama lugha ya ukombozi hasa Kusini mwa Afrika na hivyo ilichangia sana kuleta Uhuru na Umoja."

Pia, akafafanua namna lugha hiyo ilivyotumika kujenga umoja wa kitaifa na mshikamano kutatua migogoro katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Akizungumzia Kiswahili na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG), Rais huyo wa Tanzania, akasema lugha iliyokuwa nyenzo muhimu kwenye utekelezaji malengo hayo kuelekea mwaka 2030 na ajenda za Umoja wa Afrika (AU) ya mwaka 2063.

"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliunga mkono Azimio la Umoja wa Mataifa lenye namba A/76/L57 la mwezi Mei mwaka 2022 kuhusu lugha nyingi, yaani 'multilingualism', anatamka na kuendelea kuwa:

"Lilisisitiza umuhimu wa Umoja wa Mataifa, kuzipa kipaumbele lugha ambazo sio rasmi katika umoja huo kama vile Kiswahili hii ni kwa kuhakikisha lugha kama vile Kiswahili inawafikia watu wengi zaidi duniani."

Anasema, maadhimisho hayo yataendelea kuadhimishwa kila mwaka kama ishara ya kutambua umuhimu wa lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano ya kimataifa, inayokuza ushirikiano wenye mchango katika nyanja mbalimbali za amani, umoja na maendeleo ya mwanadamu.

Amewasihi Watanzania kuitumia lugha na siku hiyo kutangaza utamaduni wao.

**MTAJI UNAVYOKUA**

Hadi sasa kinatajwa, Kiswahili ni kati ya lugha zinazokua kwa kasi duniani, pia imo katika orodha ya lugha 10 zinazozungumzwa zaidi duniani na watu wasiopungua milioni 200, vilevile inafundishwa katika vyuo vikuu vikubwa vingi duniani.

Eneo lingine analitaja ni kutumika katika vituo vya redio, televisheni na vituo mbalimbali vya kutangazia duniani. Mfano wa vyombo hivyo ni pamoja na radio za kimataifa za China na Japan.

Aidha, Kiswahili kinapewa sifa kuwa ni lugha ya kwanza ya Afrika kutambuliwa na Umoja wa Mataifa kupitia UNESCO, ambao ndio waliotenga siku ya Julai 7, kuwa ya kuadhimishwa kimataifa.

Aidha, kuna wasifu, Kiswahili ndio lugha ya kwanza ya Afrika kutumika katika shughuli rasmi za Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

## BIASHARA

MBADALA KATIKA MCHUANO SOKONI...

# Namna gani unaifahamu biashara ya kuasili, inavyomudu ushindani na hatari ya hasara?

• Vigezo na masharti; mwanzo jozi ikamilike kisheria, kibiashara

**Na Aidan Mbuguye**

SIKU moja nikiwa nimeketi sehemu fulani napunga upepo huku nikifurahia muda wa kukaa peke yangu, pembeni wakaja wanaume watatu wakaketi, wakaagiza vinywaji na kuanza maongezi.

Kwa vile walikaa karibu baadhi ya maongezi yao yalinifikia moja kwa moja. Nilijitahidi nisisikie, ili kulinda utulivu wangu, lakini walikuwa wakiongea kwa sauti za juu na baadhi ya maongezi yao kunifikia.

Niligundua kuwa ni marafiki wa kawaida na urafiki wao walitaka kuhamishia pia kwenye biashara, kwa kutaka kuingia kwenye ubia au kampuni na wawili kati yao, walikuwa na hofu kuhusu mafanikio yao kibiashara.

Baadhi ya sentensi zilizonifikia ni kwamba 'je biashara yetu itafanikiwa', mwingine akauliza 'je itachukua muda kiasi gani biashara yetu kuanza kuingiza faida' na 'je tutumie njia zipi biashara yetu kujulikana na kutamba sokoni'.

Walikuwa wakibishana kiasi, huku wakionekana kuwa na hofu ya kupata hasara, isipokuwa mmoja wao ambaye alionekana kuamini katika biashara.

Kwa vile walikuwa wakiongea kwa sauti kubwa na kuathiri utulivu wangu, ikanipasa nisogee pembeni zaidi, huku nikitafakari namna wanaume hao wanavyobishana kwa hofu ya kupata hasara kwenye biashara wanayotegemea kuanzisha.

Ndipo nikawaza kuwa laiti kama wanaume hao wangewaza kufanya biashara ya kuasili basi hofu zao zisingekuwapo.

Nimeanza kwa kueleza kisa hicho kwa lengo la kuonyesha kuwa wajasiriamali wengi hawana

taarifa kuhusu biashara ya kuasili; kwa sasa duniani kote wajasiliamali wengi hufanya biashara ya kuasili na inawapatia faida.

Jamii ya wajasiriamali nchini, inapaswa kutambua kuwa si lazima uanzishe biashara yako mwenyewe, bali unaweza kuasili biashara ambayo imeshafanikiwa sokoni.




Hoteli mojawapo ngazi ya kitalii iliyoko Marekani, ambayo imepatikana kwa mfumo unaofanana na maudhui ya makala kuasilishwa. **PICHA: MTANDAO**

**MAANA YAKE**

Je Biashara ya kuasili almaarufu kwa neno la kingereza 'Franchise' ni nini? Ni idhini inayotolewa kwa makubaliano maalumu aidha na serikali au kampuni kubwa iliyofanikiwa kibiashara kwa mtu, kikundi au kampuni ndogo kutumia jina la biashara, alama, siri, sifa na manufaa mengine kufanya biashara.

Biashara ya kuasili inatakwa na wataalamu biashara, kuwa ni njia bora na yenye ufanisi kwa wajasiliamari kuanzisha biashara, hususani kwenye kipindi hiki chenye ushindani mkubwa wa kibiashara.

Wajasiliamali wengi wamekuwa wakikata tamaa na kuachana na biashara zao kwa sababu ya ugumu na ushindani wa bidhaa sokoni. Kumekuwapo ugumu kwa bidhaa mpya kupenya sokoni hususani katika kipindi hiki ambacho kuna biashara maarufu na zenye utawala sokoni.

Hakuna sababu tena ya kuhangaika, pia hakuna sababu ya kukata tamaa. Suluhisho ni biashara ya kuasili, kama hatua mojawapo.

Biashara ya kuasili, huhusisha pande mbili; Mkodishaji (Franchiser) na Mkodishwaji (Franchisees).

**MKODISHAJI NA MKODISHWAJI**

Mkodishaji; ni kampuni iliyofanikiwa katika biashara inayotoa idhini kwa wajasiliamali, kampuni kutumia jina la biashara, alama na haki nyigine kwa ada na chini ya mkataba maalumu.

Mkodishwaji; huyo ni mjasiliamali au kampuni inayopata haki ya kutumia jina, alama, siri za biashara na kufanya biashara kwa idhini na makubaliano na mkodishaji.

Faida kubwa ya kufanya biashara ya kuasili, ni kwamba mtu unapata jina la biashara ambalo tayari limeshajiimarisha na kufanikiwa sokoni, unapewa maarifa ya namna ya kuendesha na kusimamia biashara.

Anafundishwa taratibu na utaratibu wa biashara hiyo, kisha anapewa maarifa ya namna ya kusimamia na kutawala fedha, mapato na matumizi na vipimo katika biashara husika.

Kwa mujibu wa taratibu za biashara ya biashara za kuasili, mkodishwaji atatakiwa kulipa ada ya mara moja kununulia biashara hiyo (the franchise fee), pia atalipa malipo kwa kutoa mafunzo, vifaa na ushauri wa namna ya kufanya biashara husika.

Atakuwa na wajibu wa kuendelea kulipa ada ya mrabaha (the royalty fee) ambayo mara nyingi huwa inalipwa kwa wiki au mwezi na huwa inalipwa kwa hesabu za asilimia ya jumla ya mauzo. Kwa kawaida huwa ni asilimia tano hadi tisa.

Pia, mkodishwaji atakuwa na wajibu wa kusimamia biashara yake ya kuasili, faida na hasara itakuwa juu yake.

Biashara inatajwa kuwa njia bora ya mjasiliamri kuingia katika dunia ya ujasiriamali, kwa sababu ikishafanikiwa na kujiimarisha sokoni.

Vilevile, kuwekeza kwenye biashara ya kuasili inaweza kuwa ni fursa kwao, lakini kabla hajaingia kwenye biashara hiyo, ana mambo kadha aya kuzingatia.

Tathmini ya mahitaji ya soko; kuzingatia malipo ya ada mrabaha na gharama za kuanzisha biashara ya kuasili; angazia faida za biashara; na kuomba nyaraka ya biashara ya kuasili ili upate taarifa zote kuhusu biashara husika.

Eneo lingine ni kufanya uchunguzi kwanza, ili kupata taarifa sahihi kuhusu biashara inayotaka kuasiliwa; vilevile anapaswa kumshirikisha mwanasheria aliyebobea kwenye masuala ya biashara ya kuasili na mtaalamu wa masuala ya biashara na fedha

> **Tanzania imetengeneza mazingira ya kisera na kisheria yanayoruhusu biashara ya kuasili kwenye sekta tofauti, huku kuna taasisi nyingi zitokanazo na mfumo huo wa biashara.**

Hayo yanaungana na kuwapo mkataba wa biashara ya kuasili ni wa muda. Lakini haimaanishi kwamba, mkodishwaji ni mmiliki wa biashara moja kwa moja. Hapo inategemea na aina ya mkataba zimefikiwa na pande mbili.

Lakini kwa kawaida, huwa inakuwa kipindi cha miaka mitano hadi miaka 30, yenye kipengele cha kuongeza mkataba, ikienda sambamba na adhabu, endapo mkodishwaji atakiuka masharti au kuvunja mkataba kinyume na taratibu

**VYA KUASILI VS BINAFSI**

Biashara ya kuasili dhidi ya biashara binafsi: Inataja kama mtu hataki kuendesha biashara iliyoanzishwa na mtu mwingine; ni vyema akaanzisha biashara binafsi.

Lakini, mbele yake huongozwa na tahadhari kwamba, uanzishaji biashara binafsi ina hatari ya ama kukwama, kusuasua, au kutofanikiwa, ingawa upande wake wa pili, ni kuwapo faida kimapato na hata penye mafanikio inakua katika hali chanya zaidi na mmiliki abaki muasisi.

Wasiwasi mkuu hubaki kama wa wale makomredi watatu walivyokuwa wanaumiza vichwa: "je biashara wanayobuni itafanikiwa?" kibiashara zinaripoti kwamba takwimu za kutofanikiwa kwa biashara mpya ni kubwa sana.

Kuna takwimu za kibiashara... zikiangaza biashara mpya zinadumu kwa takribani miaka miwili na kuanguka asilimia 50. Pia, zinatajwa kudumu kwa takribani miaka mitano na kisha zinaanguka.

Inatajwa, kuna fursa mbalimbali za biashara ya kuasili kama vile biashara ya migahawa, hapo inazungumziwa migahawa maarufu sehemu mbaimbali.

Mjasiriamali hii ni fursa ambayo inakuhakikishia usalama wa mtaji wako na faida katika biashara yako.

**KINACHOENDELEA NCHINI**

Biashara ya kuasili kwa sasa nchini inapoatikana kirahisi na ina matangazo mengi ya mtandaoni na kwenye tovuti za kibiashara.

Tanzania imetengeneza mazingira ya kisera na kisheria yanayoruhusu biashara ya kuasili kwenye sekta tofauti, huku kuna taasisi nyingi zitokanazo na mfumo huo wa biashara.

Taratibu za kuanzisha biashara ya kuasili nchini Tanzania, zinasimamiwa na sheria za nchi, kupitia makubaliano ya kimkataba kati ya mkodishaji na mkodishwaji, inayosimamiwa na Sheria ya Mkataba, Sura ya 345.

Pia, kuna sheria nyingine nyingi zinazosimamia biashara za kuasili kulingana na aina ya biashara. Kwa kutaja kadhaa kuna: Sheria ya Kodi ya Mapato; Sheria ya Kodi Ongezeko la Thamani (VAT); Sheria ya Uwekezaji Tanzania; Sheria ya Ushindani wa Kibiashara; Sheria ya Viwango vya Bidhaa na Huduma n.k

Mkataba wa kuasili unakuwa na vipengele vya haki na wajibu kwa kila upande, kulingana na aina ya uhusiano wa kibiashara ulioanzishwa.

Mara nyingi mkataba wa kuasili unakuwa na mashariti yafuatayo: Usawa kwenye biashara, kwa mkodishaji kutaka kutawala biashara kwa thamani ya biashara, vilevile ikimtaka anayekodishwaji kuwa na mwendelezo wa kusimamia biashara yao na kulinda uwekezaji wao.

Pia, kiuna suala la mazingira ya pande zote mbili kupata faida; kufikia mahitaji na matakwa ya wateja wa kwenye biashara husika, ikihusisha hata kufanyika mabadiliko kama wateja watahitaji.

Kuna suala la kulinda maslahi ya wadau wenye maslahi katika biashara husika.

**CHANGAMOTO ZAKE**

Kwanza, inatajwa kuathiri na kupunguza ubunifu wa mjasiriamali; pia, hutawaliwa na msukumo kutoka kwa mkodishaji na kutaka kuendeleza ushindani sokoni unaolinda hadhi na sifa ya biashara yao.

Tatu, kuna utawala wa mkodishaji kwa mkodishwaji ili asiharibu jina la biashara. (brand).

**•Ni uchambuzi binafsi wa mwandishi, wakili wa sheria, Anapatikana kwa simu: + 255 759447946 na baruapepe: joranherman95@gmail.com**

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wako wapi bodaboda walioenda mafunzo ya kikazi jijini Kigali?





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008 barua pepe:kulangwasos@gmail.com

WABONGO waachwe tu waendelee kuitwa Wabongo, kutokana na bongo zao zilivyo na wazitumiavyo wakiwa Bongo, katika kuendeleza maisha yao na kujitafutia maendeleo kila kukicha.

Zamani tukiambiwa kwamba kuna mataifa hususan ya Afrika, yalikuwa yakija kujifunza mambo mbalimbali kwenye taifa hili, lililopata uhuru wake mwaka 1961 kutoka kwa mkoloni Mwingereza.

Utaratibu huo ulitokana na jinsi Rais wa Kwanza wa Taifa hili, Julius Nyerere, mjukuu wa Burito, alivyokuwa akiaminiwa, lakini kutokana na imani yake, pia kuwa asingefurahi kujitapa Tanganyika iko huru, wakati mataifa jirani yakiwa chini ya ukoloni bado.

Kwa kweli ndiyo sababu akasema, alikuwa tayari kusubiri nchi kupata uhuru mpaka mataifa mengine jirani, nayo yawe tayari kuupata, lakini likatokea la kutokea, tukawahi kuupata kabla ya Kenya na Uganda, ambao baadaye wakaja kuwa washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lakini hata baada ya kupata uhuru, mataifa yote ya Afrika Mashariki, kuna baadhi walikuwa wakija kujifunza na kuchukua mawazo yetu na kwenda kuyatekeleza kwao, hata sisi kubaki tunawakodolea macho, kwa jinsi walivyoingiza nadharia kwenye vitendo kwa umakini mkubwa.

Hivi mnajua kuwa majirani zetu Wanyarwanda walijifunza mengi sana kwetu? Acha Msumbiji, Zambia, Zimbabwe, Afrika Kusini hata Angola na wengine wakikita kambi nchini, kupambania uhuru wao huku wakiiga umoja na mshikamano tuliokuwa nao Watanganyika, baadaye Watanzania!

Kuna Wanyarwanda tulikuwa nao katika kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kuna waliokuwa viongozi katika taasisi zetu za kiserikali na kiraia na baadaye tukajawaona wakiwa viongozi katika taifa lao la Rwanda.

Si Uganda na kwingineko katika maeneo haya ya Afrika, kuna wageni walikuwa nchini mwetu wakijifunza mengi na kwenda kuyatumia kwao kwa manufaa makubwa kwa mataifa yao. Sisi tunaweza hayo? Yaani kujifunza nje na kuja kutumia hapa!

Hivi karibuni, kuna wenzetu walikwenda Cuba kwenye kitu kinaitwa Kongamano la Kiswahili, tukashuhudia kundi kutoka Bongo likiwa jijini Havana, likizungumza na kuhanikiza Kiswahili, lilikwenda kueneza lugha hii adhimu.

Nasikia wamerudi, lakini halijatwambia mafanikio ya ziara hiyo na kama kweli watu huko walihamasika na kuanza kutumia Kiswahili, mbali na kukipenda kama tunavyokipenda hapa ingawa baadhi kimachale!

Tunatambia Kiswahili, lakini hatukitumii, tunakitambia lakini hatuonyeshi kukipenda. Leo hii tunasikiliza redio zetu na luninga watangazaji na wachambuzi wanazungumza Kiswangilishi, wakiamini kufanya hivyo ndio kuonyesha umahiri wa mambo!

Ukikosea ukasikiliza, siku hizi kuna vipindi vya wachambuzi hususan wa michezo, wanazungumza mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, utashangaa na hiyo inatokana na hata vipindi yenyewe kuitwa majina ya Kiingereza.

Na vingine vingi tu, majina ya kigeni! Mjadala unaendeshwa kwa lugha ya kienyeji; Kiswahili! Unajiuliza hivi majina ya vipindi yakiwa ya Kiswahili umahiri unajificha au kitu gani?

Tukiendekeza hili, basi ipo siku tutaamka asubuhi magazeti yote ya Kiswahili yana majina ya Kiingereza lakini habari za Kiswahili, kama ndiyo lugha inaonyesha umahiri wa mawasiliano katika jamii ya Kibongo.

Acha hilo, hivi karibuni nikaipata nyingine mpyaa, mpya kabisa! Eti kwamba serikali kama ilivyopata kufanya kwa wasanii wetu kuwapeleka Seoul, Korea Kusini kujifunza, imepeleka madereva wa bodaboda Kigali, Rwanda, kujifunza nidhamu ya barabarani katika taifa hilo changa kwa Tanzania.

Aliyenimegea ubuyu huu, hakuniambia walichukua siku ngapi za mafunzo Kigali, lakini naambiwa tu walimaliza mafunzo na kurejea nchini. Hakuna hata moja wanatekeleza kati ya waliyojifunza huko, angalau hata kuheshimu taa za kuongozea vyombo vya moto barabarani.

Kama si hilo, basi angalau kukumbuka kuvaa kofia za chuma wawapo barabarani wakiendesha mapikipiki yao hayo, je, la kusubiri kwenye kivuko cha pundamilia ili waenda kwa miguu wapite! Lakini badala yake, bodaboda ndiye anavuka kwenye pundamilia, kuingia barabara ya mabasi yaendayo haraka!

Hivi sasa ukikaa barabarani uangalie uchafu wanaoufanya bodaboda, unajitapikia mwenyewe kama mlevi wa gongo walahi. Yanafanyika huku polisi wa usalama barabarani wakishuhudia kana kwamba hawawaoni.

Unajiuliza hivi ni kwa sababu walipunguziwa na Bunge faini kutoka Sh.30,000 kwa kosa hadi Sh 10,000, eti kwa madai hawana kipato au kwa kuwa Chifu Hangaya aliwabatiza jina la 'Maofisa Usalama' hivyo kukwea kileleni mwa sheria na kuzitazama kwa chini? Oriti Yawa!

BIASHARA

MAISHA MAPYA KWA WAKULIMA 100...

# Mradi pampu maji, umeme wawazawadia walima mboga mtoni Kisarawe na Rufiji



Mradi wa umwagiliaji shambani Pwani; kutoka kushoto ni chanzo cha nishati; katikati ni mabomba ya kumwagilia shambani; na kulia ni maeneo maji yanapochukuliwa mtoni. **PICHA ZOTE: GRACE MWAKALINGA**

**Na Grace Mwakalinga**

JUA lilikuwa linazama kwa upole katika vijiji vya Cholesamvula na Kwara katika wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, kuna wakulima wa mboga na matunda kwa nyakati tofauti wamekusanyika pembezoni mwa mashamba yao wakisherehekea maji yanayobubujika kwa urahisi kutoka kwenye pampu inayotumia nishati ya umeme wa jua.

Hiyo ni ishara ya mabadiliko makubwa yaliyosababishwa kupitia mradi uitwao PPP (People, Planet, and Prosperity), unaotekelezwa mahali hapo.

Kwa sasa ni vijiji vinne tu katika halmashauri za Kisarawe na Rufiji, ambazo zimefungiwa miundombinu ya nishati umeme jua, kwa maana ya pampu zinazosukuma maji kutoka mto Rufiji hadi kwenye mashamba yao.

Hapo kuna vijiji vya: Mtanzamsona, Mloka, Kipo, Chole - Samvula na Kwara, ambako wakulima wamejengewa miundombinu hiyo ya umeme wa jua.

Matumizi ya nishati hiyo ni katika kumwagilia na tayari wanataka kuyaona mapinduzi makubwa kimaisha kwao wakulima, wanapata maji kirahisi kijijini, kwa gharama nafuu na mazingira rafiki, pia ikiwaongeza faida ya uzalishaji mazao.

Halima Ally kutoka Kwara, anayelima bustani za mboga, anasema pampu zinazotumia umeme wa jua zimemhamisha kuondokana na matumizi ya mafuta ya petroli na dizeli kwa genereta kumwagilia shambani.

"Imenisaidia kuongeza uzalishaji wa nyanya na pilipili, sipo tayari kutumia teknolojia nyingine kwa sababu sihitaji tena kuacha shamba langu likikauka wakati wa kiangazi," anasema Halima.

Moses Alphonce, anayejishughulisha na bustani, anasema nishati hiyo imekuwa suluhisho kwake, kwani alitegemea mvua, sasa anaweza kumwagilia shamba lake mwaka mzima, ikimuwezesha kupata mazao mara mbili kwa mwaka.

"Nimeongeza eneo la kulima kutoka ekari mbili hadi tatu, natarajia msimu huu wa mavuno nitapata mara mbili ya mavuno ya msimu uliopita," alisema Alphonce.

Asha Juma, anayelima mahindi na mihogo, anasema sasa ana uwezo kusambaza maji shambano kote, mazao yake yalisitawi pia akipata mavuno zaidi.

Hapo anataja mfano wa zao la manufaa - tikitimaji, akijinasibu ana muda mwingi wa kukaa na familia yake, kwa kwa sababu ana uhakika wa maji shambani.

Fatuma Rahim, ni mama wa watoto wanne, anayefurahia mageuzi hayo ya nishati ya jua, ikibadilisha Maisha, mwenyewe akiitafsiri:

"Kilimo kimekuwa cha kisasa zaidi, anasema hakuna tena changamoto ya ukosefu wa maji wakati wa kiangazi, sasa nimeweza kupeleka watoto shule kwa kutumia mapato ya kilimo."

Anaendelea: "Teknolojia ya umeme jua si tu kwamba inaongeza tija kwa wakulima bali pia inalinda mazingira kwa kupunguza utegemezi wa mafuta ya dizeli."

**WAENDESHA MRADI**

Thomas Mkunda, ni Mratibu Msaidizi wa Mradi wa PPP kutoka Shirika la Tangsen, anasema unalenga kuwawezesha wakulima kupitia masuala ya jinsia na nishati wakazalisha mazao rafiki na mazingira yao.

Anasema, kuna wakulima zaidi ya 100 wanaoondoka kwenye utegemezi wa mafuta ya dizeli na petroli na kuhamia mbadala rahisi kwao kimazingira.

"Kwa kutumia pampu zinazotumia umeme wa jua, wakulima wanapata maji kwa urahisi na kwa gharama nafuu, na pia wanachangia katika uhifadhi wa mazingira," anaeleza Mkunda.

Mkunda anasema, kabla ya kuweka miundombinu hiyo, walianzs na kuwaelimisha wakulima, lakini wakawa na wasiwasi wa tija itokanayo na nishati hiyo mbadala ya kisukuma maji kutoka mtoni hadi mashambani.

Hata hivyo baada ya kuona mafanikio ya pampu hizo, wengi wamekubali na kujiunga nazo, wakiamini ina tija zaidi ya nguvu ya dizeli.

Anataja gharama za kununua mafuta ya dizeli na petroli kwa za pampu za maji, mkulima anatumia shilingi 15,000 za lita tano za petroli na wengine hukodi pampu kwa shilingi 10,000 kwa siku, hivyo kuwaingizia bajeti ya 25000.

Mkunda anasisitiza kuwa, pampu za umeme wa jua ni mbadala unaomwokolea mkulima gharama kubwa, huku kimazingira inanusuru kasi kubwa ya kusambaza hewa ya ukaa, hatari kwa mazingira na afya za binadamu.

Anawataja kinamama kuwa wanufaika zaidi wa mradi, kwani wao ndio kwa kiasi kikubwa wanajihusisha na kilimo, hivyo teknolojia hiyo mpya ni manufaa kwao.

"Tunatarajia kwamba wakulima wengi wataweza kununua pampu hizi baadaye, vijiji vingi vilivyo pembezoni mwa mto vina fursa ya kutumia nishati ya umeme jua kwa ajili ya kupampu maji na kumwagilia mashamba yao. Hata kwa wale ambao hawajaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa," anasema Mkunda.

Anaeleza, katika huduma za ziada wanazotoa kwa wakulima hao kwenye mradi, ni ushauri wa kitaalam, kuwaunganisha na nishati hiyo, pia kuwafundisha utaalamu wa Kutumia maji, ili wapate matokeo bora katika umwagiliaji.

Akizungumzia kuhusu gharama za kununua vifaa hivyo, ambazo ni shilingi milioni mbili hadi tatu, wakulima hupewa mbadala kujiunga katika kikundi cha watu 15 kikijiunga wanunua mashine na kutumia kwa pamoja, ikiweza umwagilia shamba lenye ukubwa wa ekari tano kwa wakati mmoja, maji yakitumiwa kwa ufanisi.

Anataja maeneo mengi ya mashamba hayajafikiwa na nishati ya umeme wa gridi ya taifa, wakulima hao wanaweza kutumia fursa hiyo kupata pampu, kama mbinu mbadala.

Secilia Bongote, Mkufunzi wa katika mradi huo, wilayani Kisarawe, anasema wanawake wanashiriki kwa kiwango kikubwa katika kilimo cha mboga, matunda na miti na sasa wanapata manufaa zaidi kutokana na teknolojia ya umeme wa jua.

Anawasifu kujitahidi kwao kuwa sehemu ya mabadiliko hayo kwa kujifunza na kutumia teknolojia hiyo ikiwasaidia kuongeza uzalishaji, kuokoa muda na nguvu, na hivyo kuboresha kipato cha familia zao.

Mkufunzi wa mradi wilayani Rufiji, Justas Muganyizi, anasema awali wakulima walikuwa wanalima maeneo madogo kwa ajili ya kupata chakula, lakini kwa kushirikiana na serikali, wamewahamasisha kulima maeneo makubwa.

Anasema jitihada hizo za kuwahamasisha kulima eneo kubwa, zimeendana na kuwahimiza kutumia pampu za umeme wa jua katika mradi huo, zikiwa zimefungwa katika vijiji vya Mloka na Mtanzamsona na uzalishaji wa mboga umeongezeka kwa asilimia kubwa.

Anasema hadi kufikia mwaka 2025, wanatarajia uzalishaji wa mboga kufikia tani 20, watafanikiwa kwa sababu wamewajengea uwezo wakulima kuzalisha kibiashara.

Ofisa Biashara na Masoko wa Shirika la Kimataifa la Transform Trade, Sebastian Mahenge, anasema ni mradi unaowsaidia wanajamii kuimarisha shughuli zao kiuchumi, kwa kutumia mbinu rafiki na kisasa, endelevu kwa ajili ya kutunza mazingira.

Anasema mbinu hizo ni pamoja na kuwaunganisha katika vikundi vya kiuchumi kwa ajili ya kupata masoko hatua inayowapa fursa ya kuuza bidhaa zao kwa bei nzuri na hivyo kuongeza kipato.

Anafafanua kuwa lengo la mradi lilikuwa kuwafikia wakulima 2,200, lakini hadi sasa tumewafikia wakulima 2,548, kati yao 1,308 ni wanawake na 1,240 ni wanaume.

Anaongeza kuwa mradi ulikuwa na lengo la kuwafikia wakulima 100 wenye ulemavu, lakini umewafikia wakulima 110, na wakulima wote 2,548 wamejiunga na vikundi mbalimbali vya kiuchumi, vinavyowawezesha kushirikiana katika kukuza uzalishaji na kuboresha maisha yao kiuchumi.

Anaongeza kuwa mradi huu pia unalenga kupunguza uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchomaji wa mkaa, ambao umekuwa tatizo kubwa katika wilaya za Kisarawe na Rufiji.

Anasema Mradi wa PPP ulianza mwaka 2022 na unatarajiwa kukamilika Machi 2025, kwa kushirikiana na shirika la Tangsen ambalo lina utaalam katika nishati na jinsia.



# Watumishi wajengewa nyumba 200

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, anatarajiwa kuzindua zaidi ya nyumba 200 kwa ajili ya watumishi wa umma jijini hapa Jumatano ijayo na kuwawezesha kumiliki kwa masharti nafuu.

Akizungumza jana jijini hapa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema nyumba hizo zimejengwa chini ya Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma (WHI).

Senyamule, Dk. Mpango atazindua nyumba hizo Desemba 11, mwaka huu katika eneo la mradi la Njedengwa.

Alisema Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia taasisi yake WHI kwa kushirikiana na ofisi yake imeandaa uzinduzi huo.

"Hafla hii pia ni fursa ya kuonyesha mshikamano wa kitaifa kutatua changamoto za makazi na kuimarisha ustawi wa jamii," alisema.

Senyamule, alisema viongozi wa serikali, wadau wa maendeleo na wananchi watahudhuria uzinduzi huo.

**"Hafla hii pia ni fursa ya kuonyesha mshikamano wa kitaifa kutatua changamoto za makazi na kuimarisha ustawi wa jamii," alisema.**

"Utekelezaji wa mpango wa makazi kwa watumishi wa umma ni dhamira pana ya serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata fursa ya kumiliki makazi bora," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Mtendaji Mkuu wa WHI, Dk. Fred Msemwa, alisema nyumba hizo 206 ni kati ya 1,000 zilizojengwa katika mikoa 19 nchini ili kuwawezesha watumishi wa umma kumiliki makazi bora, kuboresha utendaji kazi na kuleta ufanisi kwa taifa. Tangu kuanza kwa mpango huo mwaka 2014 hadi sasa, zaidi ya nyumba 1,000 zimejengwa katika mikoa 19.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni pamoja na Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Simiyu na Mtwara.

Alisema kupitia mpango huo, wametoa mikopo yenye masharti nafuu kwa watumishi wa umma kuwawezesha kumiliki nyumba kwa urahisi zaidi.




Mwenyekiti mstaafu wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Salome Kitomari (kushoto), akimpongeza Mwenyekiti mpya wa Taasisi hiyo, Edwin Soko baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Singida kuanza mwaka kwa gesi ya bei chee

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI inatarajia kutoa mitungi ya gesi 19,530 ya ruzuku kwa Mkoa wa Singida na kuuzwa kwa bei ya chini kwa wananchi waishio vijijini mwanzoni mwaka ujao.

Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego, aliyasema hayo juzi baada kuwapokea maofisa kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mahususi kwa ajili ya kutekeleza mpango huo.

Dendego, alisema maofisa hao wamewasili mkoani hapa kwa ajili ya kupeleka mradi wa usambazaji wa mitungi hiyo ya gesi yenye ruzuku.

Alisema mitungi hiyo itagawanywa kwa uwiano sawa kwa wilaya tano za mkoa huo ili kuhakikisha wananchi wa vijijini wananufaika.

Alisema ujio wa mradi huo ni faraja kwa wakazi wa Singida kutokana na takwimu kuonyesha asilimia 20 tu ndio wanaotumia nishati safi ya kupikia.

Mkuu huyo wa mkoa, alisema kiwango hicho ni kidogo sana ikilinganishwa na kaya zilizopo mkoani kwake na kwamba inaonesha idadi kubwa ya wananchi wengi wanatumia nishati chafu kwa kupikia kuni na kuchangia uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

"Mkoa wa Singida tulishaanza kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi kupikia, kwa hiyo hili ambalo REA mumetuletea ni habari njema sana hasa ikizingatia kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakiomba bei ya mitungi ya gesi ipunguzwe, nampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuja na suluhisho," alisema.

Awali Mhandisi Mwandamizi kutoka REA, Deusdedit Malulu, alisema mradi huo kwa mkoa huo utaanza kutekelezwa Januari mwakani.

Malulu, alisema mitungi hiyo kila mmoja utakuwa na ujazo wa kilo sita na kwamba serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 8.6 kutekeleza mradi huo kwa mkoa huo.

Alisema mradi huo unatekelezwa nchi nzima kwa kusambaza mitungi 452,000 katika mikoa yote.

Alisema mtungi mmoja utauzwa kwa bei ya ruzuku Sh.20,000 badala ya Sh.40,000 hadi 45,000 za awali kulingana na umbali kutoka jijini Dar es Salaam.

Malulu, alisema kwa Singida kila wilaya itapewa majiko 3,255 na kwamba idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na kaya zilizopo.

Alisema kwa mkoa huo, huo ni mradi wa majaribio kwani kutakuwa na mingine kutegemea bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

# Wakulima washauriwa kukabili njaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKULIMA wa Kanda ya Kati wamehamasishwa kupanda mazao yanayostahimili ukame ili kukabiliana na upungufu wa chakula.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT), Julius Bundalla, alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na waandishi habari jijini hapa baada ya mvua kuanza kunyesha katika baadhi ya mikoa nchini.

Mchungaji Bundalla, alisema kutokana na maeneo ya Kanda ya Kati kupata mvua za wastani kila mwaka, kuna umuhimu wakulima kuwatumia wataalamu wa kilimo na kuzingatia mbegu bora za mazao zinazostahimili mvua hizo.

Kwa upande mwingine, aliwaasa viongozi waliochaguliwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji hivi karibuni, kuwatumikia wananchi bila ubaguzi.

Bundalla, alisema viongozi hao wasigeuze madaraka yao kama mtaji wa kujipatia rushwa kutoka kwa wananchi wanapohitaji kupata huduma.

Alisema wananchi wanatarajia kuona maendeleo kwa vitendo kwa faida yao wenyewe.

# Ofisi ya CAG yashauriwa kuchochea usawa jinsia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTANDAO wa Jinsia nchini (TGNP), umeishauri Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi na kuchochea usawa wa jinsia nchini.

Mwezeshaji kutoka TGNP, Mary Nsemwa, alitoa ushauri huo jana jijini hapa kwenye kikao kazi baina ya Menejimenti ya ofisi hiyo kujadili masuala ya kuzingatia wakati wa ukaguzi.

Nsemwa, alisema lengo ni kuzingatia usawa na kuwa na mtazamo wa kijinsia wakati wa uandaaji mipango, miongozo na kazi za ofisi hiyo.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa sababu yanashirikisha uzoefu wa taasisi kwenye masuala ya kijinsia na kuweka mikakati ya kuboresha maeneo muhimu," alisema Nsemwa.

Alisisitiza kuwa ofisi hiyo itafanya ukaguzi kwa usawa na haki kwa makundi ya wanawake na yenye uhitaji maalum ili kuyaletea maendeleo.

Hata hivyo, alisema kaguzi hizo zinapaswa kuzingatia sera, miradi, huduma za serikali na kuondoa tofauti za kijinsia kwa wanawake na wanaume.

Nsemwa alitaja maeneo mengine yanapaswa kuangaliwa wakati wa ukaguzi kuwa ni uwiano wa bajeti kwenye miradi inayotekelezwa na serikali nchini.

Degratius Temba kutoka TGNP, aliitaka jamii kutambua usawa uko kwenye elimu, afya, maji na jamii.

Temba, alisema Tanzania inazingatia miongozo ya usawa wa kijinsia na kuibua vipaumbele katika jamii kwa manufaa ya makundi hayo. Alisisitiza mgawanyo wa kazi katika jamii kwa kuzingatia jinsia na kuishawishi kushiriki katika maendeleo na kujiingizia kipato.

Alisema kutotekelezwa kwa baadhi ya miongozo ya usawa wa kijinsia ni moja ya tatizo katika jamii kutokana na mila, desturi na tamaduni.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Benja Majura, alisema mafunzo hayo ni chachu kwao kuzingatia jinsia na kuongeza uelewa wa kuandaa bajeti.





# Wakulima wa chai watangaziwa neema ya masoko

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Chai Tanzania imeanza kurejesha masoko ya chai yaliyopotea, lengo likiwa ni kukabiliana na matatizo wanayokumbana nayo wakulima.

Kaimu Mkurugenzi wa bodi hiyo, Beatrice Banzi, alisema hayo jijini Dar es Salaam baada ya kutembelewa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Kimataifa ya Chai Omani, Khalfan Abdullah.

Alisema zamani walikuwa wananunua chai hapa nchini lakini baadaye waliacha kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema katika mazungumzo yao ya kuwarejesha upya wameahidi kununua tani 100 za chai kwa mwezi na kwa mwaka tani 1,200.

Beatrice alisema hatua hiyo itasaidia kumaliza kilio cha wakulima wa chai Mponde wilayani Lushoto mkoani Tanga cha kukosa soko.

"Wamesema Desemba 15 mwezi ujao wataanza kununua chai, nimepokea kwa sura ya furaha ahadi yao, tumeanza kufungua njia kwa masoko yaliyofungwa na kupata mengine mapya.

"Hili ndio lengo la Bodi ya Chai, Wizara ya Kilimo na serikali kwa ujumla ni kuona tatizo la soko la chai nchini linafikia ukomo. Wakulima wasikate tamaa bodi ya chai ipo inaendelea kutafuta masoko ndani na nje ya nchi, ili kuwasaidia kuuza mazao yao kirahisi," alisema Beatrice.

**"Wamesema Desemba 15 mwezi ujao wataanza kununua chai, nimepokea kwa sura ya furaha ahadi yao, tumeanza kufungua njia kwa masoko yaliyofungwa na kupata mengine**

Alisema mbali na kuwarejesha wanunuzi hao kutoka Oman wameanza kurejesha soko la Sudan akikumbushia kuwa siku chache zilizopita walikwenda ubalozi wa nchi hiyo kwa ajili ya kuangalia namna ya kutanua soko la bidhaa hiyo mahali huko.

Aliongeza kuwa serikali tayari imeagiza mashine kwa ajili ya kujenga viwanda vya kuchakata chai, akisema hatua hiyo kutasaidia kupunguza changamoto ya soko kwa wakulima.

Aidha, aliwataka wakuu wa kampuni, mashirika na vyama vinavyojihusisha na masuala ya chai kuendelea kuwatembelea wakulima wa chai ili kusikiliza na kutatua kero zao.

Ofisa Masoko wa bodi hiyo, Selemani Chilo alisema kufufuka kwa soko la chai Oman kutaisadia Tanzaia kuingiza Dola za Marekani milioni 1.5 kwa mwaka (Sh. bilioni 3.9).



Rais wa Lions Klabu Dar es Salaam Infinity, Priscilla Alva (wa nne kushoto), akikabidhi sehemu ya madawati 300 kwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Mtinka, yaliyotolewa mchango na klabu hiyo kwa Shule ya Msingi Mbagala juzi, ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuongeza upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wa kitanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu elimu ya juu watakiwa kutochagua kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHITIMU wa vyuo vikuu wametakiwa kuendelea kujifunza mambo mapya ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani ambayo yatawasaidia kujiletea maendeleo na taifa.

Pia, wametakiwa kuacha kuchagua kazi na badala yake wafanye kazi yoyote halali ya kuwaingizia kipato, zikiwamo kazi za kujiajiri na kuacha kulalamikia ukosefu wa ajira

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Ally Mohamed Shein, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya 23 ya chuo hicho ndaki ya Mbeya ambapo aliwataka wasibweteke baada ya kuhitimu shahada zao.

Alisema kuna baadhi ya wahitimu wa vyuo vikuu wamekuwa wakikosa ajira kutokana na kutojituma kwa sababu ya kuwa na fikra potofu za kutegemea ajira serikalini pekee. "Kwa sasa dunia imebadilika, dunia ilivyo sasa ni tofauti na itakavyokuwa mwaka 2050, kutakuwa na mabadiliko mengi ya teknolojia na baadhi yenu mtafika huko, kwa hiyo ili mwendane na mabadiliko hayo hakikisheni mnajiendeleza kwa kusoma," alisema Dk. Shein.

Dk. Shein alisema kwa sasa serikali inawategemea wasomi wa vyuo vikuu kusaidia kwenye maeneo mbalimbali ya maendeleo.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Mzumbe, Prof. William Mwegoha, alisema chuo hicho pamoja na maendeleo mbalimbali ambayo kimepata lakini kinakabiliwa na uhaba wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi, hali ambayo inasababisha wengi wao kuishi nje ya chuo.

Alisema kwa sasa uongozi wa chuo hicho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wameanzisha harambee kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hosteli za wanafunzi hasa kwa ajili ya wanafunzi wa kike ambao ndiyo wanakabiliwa na matatizo mengi.

Alisema ili kukamilisha ujenzi wa bweni hilo wanahitaji zaidi ya Sh. bilioni tano lakini mpaka sasa wamekusanya Sh. milioni 90 pekee hali ambayo inachelewesha kuanza kwa mradi huo.

Alisema fedha hizo zimechangwa na wadau mbalimbali wakiwamo wanafunzi waliohitimu chuo hicho miaka ya nyuma pamoja wadau wengine wa maendeleo.

"Tulipokuwa kwenye mahafari kama haya kule Morogoro Rais Samia Suluhu Hassan aliguswa na tatizo hili la uhaba wa mabweni na alituahidi kutushika mkono, lakini tunaomba wadau waendelee kujitoa ili tukamilishe mradi wetu," alisema Prof. Mwegoha.

Alisema chuo hicho kina wanafunzi wengi lakini wanaokaa hosteli za chuoni ni wachache na hivyo kusababisha idadi kubwa kuishi nje ya chuo hasa kwenye makazi ya watu binafsi ambako wanakumbana na matatizo mbalimbali.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa chuo hicho, Prof. Saida Yahya, aliipongeza serikali kwa kuanza kubadili mitaala hasa kwa kuanza kuimarisha mafunzo ya vitendo akidai kuwa mitaala hiyo itasaidia kupunguza tatizo la ajira.

# DC: Uchaguzi umeisha tushike jembe tukalime

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, amewataka wananchi wilayani humo kuelekeza nguvu kwenye msimu mpya wa kilimo na kuacha kufikiria siasa kwa maelezo kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa umemalizika.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akitoa shukrani kwa viongozi wa dini wa madhehebu mbalimbali ofisini kwake.

"Uchaguzi umeisha na sasa mawazo yote wananchi tuelekeze kwenye uzalishaji wa kilimo. Ni msisitizo wetu sisi serikali, na niwaombe viongozi wa dini tuangalie kitu gani kinafuata baada ya huu uchaguzi kwamba tuendelee na shughuli zetu za kawaida," alisema Kissa.

Alisema Mungu amesaidia uchaguzi umeisha watu wakiwa imara na wamoja bila ya kutokea matukio ya kuhatarisha amani.

"Njombe ipo salama na amani, Mungu amekuwa ni mwema lakini ni kwa sababu viongozi wa dini na wananchi tuliweza kuungana kwa pamoja na nyinyi wenzetu mliweza kumwomba Mungu na sisi waumini wenu tulisikiliza maono ambayo mliyatoa," alisema Kissa.

Baadhi ya viongozi wa dini walisema uchaguzi ulifanyika kwa kuzingatia demokrasia na haki, huku kampeni zikiendeshwa kistarabu hali iliyosaidia kutokuwa na uvunjifu wa amani.

Wakizungumza katika kikao hicho, Askofu Msaidizi wa Jimbo la Njombe wa Kanisa la EAGT, Ibrahimu Mtonyole alisema amani yote iliyopatikana katika kipindi chote cha uchaguzi ni kutokana na maombi yaliyofanywa na viongozi wa dini usiku na mchana.

"Lakini pia tukuhakikishie sisi kama wachungaji na maaskofu tuko pamoja na serikali kuhakikisha kwamba tunaombea amani ili nchi yetu iendelee kuwa na amani na utulivu kama ulivyo uchaguzi katika sehemu nyingine tumesikia mauaji lakini sio Njombe," alisema Mtonyole.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Ushirika wa Njombe Mjini, Nelson Godiwe, alisema nchi imefanya siasa za kizalendo na wananchi wamechagua kile ambacho wameelewa.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea na ndoto ambazo wanazo kwa taifa na kwa familia zao ili kuweza kufikia hatima kwa kuwa kwenye uchaguzi lazima kukubali kwamba kuna mmoja atatangulia mbele na wengine watafuata.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki, aliwaomba viongozi wa dini kwenda kuwakumbusha wazazi kipindi cha likizo watoto wanaporudi nyumbani kufundishwa maadili.



# UN yakoshwa juhudi Jeshi la Polisi kuzuia uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Polisi Umoja wa Mataifa, Kamishna Faisal Shahkar, amesema amefurahishwa na juhudi na umahiri wa Jeshi la Polisi Tanzania Kamisheni ya Zanzibar katika kuzuia uhalifu na kuifanya Zanzibar kuwa sehemu salama.

Akizungumza visiwani Zanzibar na maofisa wa polisi, makao makuu ya Polisi Zanzibar, Kamishna Faisal alisifu namna Jeshi la Polisi linavyoshirikiana na vyombo vingine katika kukabiliana na makosa mbalimbali yakiwamo ya udhalilishaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Alisema kuwa Umoja wa Mataifa (UN) upo tayari kulisaidia Jeshi la Polisi Tanzania kwa kuliwezesha katika nyanja tofauti ili kufanikisha kuzuia uhalifu.

Naye Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alisema ziara ya kamishna huyo visiwani Zanzibar ina dhamira ya kuimarisha umoja baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na UN katika kukuza amani, usalama na maendeleo.

Alisema Tanzania inajivunia kuwa mshiriki hai katika juhudi za kulinda amani za UN polisi na wanajeshi wanaendelea kutoa huduma ya ulinzi katika nchi tofauti duniani.

**Alisema Tanzania inajivunia kuwa mshiriki hai katika juhudi za kulinda amani za UN polisi na wanajeshi wanaendelea kutoa huduma ya ulinzi katika nchi tofauti duniani.**

Alisema uzoefu huo ulimfundisha umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kushughulikia changamoto za usalama na kulinda jamii zilizo hatarini.

"Uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na Asia, hususani Pakistan, umejikita katika karne nyingi za biashara, uhamiaji na kubadilishana tamaduni. Bahari ya Hindi imekuwa daraja linalounganisha Afrika Mashariki na Asia Kusini, hivyo kukuza uhusiano uliowafaidisha wote," alisema.

Alisema Jumuiya ya Wapakistani imekuwa na mchango mkubwa katika historia ya Tanzania, hususani katika biashara, viwanda, na maendeleo ya jamii ambapo katika kipindi cha ukoloni, Wapakistani wengi walihamia Afrika Mashariki, ikiwamo Zanzibar, ambapo walichangia ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.



Mkurugenzi wa Kampuni ya JHS Enterprises Ltd, Harbinder Singh Reehal (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, alipofanya ziara ya kujionea mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya utalii iliyoandaliwa na serikali. Kushoto ni Amarjit Singh Reehal. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mariam Mwinyi awafunda wazazi kuhusu elimu

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi amewataka wazazi na walezi, kutumia fursa iliyopo kwa kuwapeleka watoto shule zilizokaribu na maeneo yao ili waandikishwe.

Alitoa rai hiyo kupitia taarifa aliyoitoa kwa umma akiwa ofisini kwake Ikulu ya Migombani, Mkoa wa Mjini Magharibi kuhusu uandikishaji wanafunzi wa ngazi ya maandalizi na msingi kwa mwaka wa masomo 2025.

Alisema watoto wote wenye umri wa miaka minne hadi mitano waandikishwe kwa ngazi ya maandalizi na watoto wote watakaofika umri wa miaka sita ifikapo mwaka 2025 waandikishwe kwa ngazi ya msingi.

Mariam Mwinyi ambaye ni Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya "Zanzibar Maisha Bora Foundation" (ZMBF), aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawachukulia vyeti vya kuzaliwa watoto wao wanapokwenda kuwaandikisha shuleni.

"Ndugu mzazi, hakikisha unapokwenda shule kumwandikisha mtoto wako usisahau kuchukua cheti chake cha kuzaliwa". alisema.

Aidha, alisema kwa sasa uandikishaji kwa shule zote za serikali na binafsi unaendelea nchini mpaka Desemba 30, mwaka huu.

Pia, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuunga mkono jitihada za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi za kuwawekea miundombinu wezeshi ya elimu kwa kupeleka watoto wote kuandikishwa na kuhakikisha hakuna mtoto atakayebakia nyumbani.

Pia, kwa shule za serikali watoto wote wataandikishwa bila ya gharama yoyote na elimu ni haki ya msingi kwa kila mtoto.

# ZFDA yaagizwa kufanya ukaguzi katika machinjio

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imeutaka Wakala wa Chakula, Dawa, Vipodozi na Vifaatiba (ZFDA) kuimarisha ukaguzi katika machinjio yote ya Unguja na Pemba.

Pia imeagiza kuweka mazingira mazuri na yenye viwango, kutoa elimu zaidi kwa wananchi juu ya athari zinazojitokeza kwa uchinjaji holela wa wanyama.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Nassor Salim Ali, alisema hayo wakati akiwasilisha maoni ya kamati hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema jukumu la msingi la ZFDA ni kusimamia udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kufanya usajili, ukaguzi, uchunguzi wa kimaabara na udhibiti wa uingiaji wa bidhaa hizo nchini.

Alisema ili ZFDA iweze kufikia malengo yake ipo haja ya kuimarisha vifaa vya kisasa vya maabara na kuwajengea uwezo wataalamu ili iweze kufikia lengo la kupata ithibati ya kimataifa.

Pia alisema ZFDA inapaswa kutoa elimu juu ya athari ya matumizi ya chupa za plastiki zaidi ya mara moja bila kuzirudisha kiwandani kwa ajili ya kusafishwa tena hasa kwa wafanyabiashara wa vinywaji kama maziwa na juisi.

Alisema kamati inaitaka pia ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuharakisha kukamilisha mapitio ya kanuni ya usajili wa bidhaa za dawa ya mwaka 2024, ili kazi ya usajili wa bidhaa hizo iweze kutekelezwa kwa ufanisi zaidi.

Hivyo, alisema kamati inaishauri ZFDA kuhakikisha kwamba mifumo hiyo inasomana na iwe inakwenda na wakati wa sasa, iwe endelevu na kufanya ukaguzi kwa wazalishaji wa ndani na nje ya nchi ili kujiridhisha kuwa bidhaa za chakula zinazoingia katika soko la Zanzibar zinazalishwa kwa ubora na usalama.

Alisema wanapaswa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa umakini kwa kuteketeza bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu na nyingine kuzirudisha zinakotoka ili kuzinusuru afya za wananchi.

Vilevile, aliitaka ZFDA iendelee na ukaguzi wa maduka na ghala za vyakula, dawa na vifaa tiba ili kujiridhisha kama vina viwango na vinafikia vigezo stahiki na kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) wanunue mitambo inayofanana ili iwe rahisi wakati wa kumuita mtaalamu wa kuifanyia matengenezo hayo kwa pamoja na kupunguza gharama.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema taasisi imefanikiwa kufanya utafiti wa kujua hali halisi ya maradhi ya ngozi yaliyoleta taharuki kubwa kwa wakazi wa Wilaya ya Micheweni.

Alisema utafiti huu umegundua kuwa wagonjwa wapatao 17 wamegundulika na maradhi ya ngozi na hatimaye elimu ilitolewa juu ya ugonjwa huo kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya ya Micheweni Pemba.

Waziri Mazrui alisema kabla ya kufanya utafiti huo wananchi walikuwa na dhana ya kuwa maradhi hayo yanasababishwa na imani za kishirikina lakini utafiti umegundua kuwa maradhi hayo ni matatizo ya vinasaba ambapo mtu huzaliwa na ngozi dhaifu inayoshindwa kupambana na mazingira ikiwamo jua na kusababisha saratani ya ngozi.

Aidha, alisema taasisi hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo tatizo la uhaba wa watafiti wabobevu wenye uwezo wa kuandika na kushinda miradi ya tafiti.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI




**TEKLA PASCAL MZIBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S2391/0065** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LUDUGA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017, Cheti NTA LEVEL 4 chenye **No. NS2391/0065/2017** Kilichotolewa **CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA** mwaka 2020 na Cheti NTA LEVEL 5 chenye No. **NS2391/0065/2017** Kilichotolewa **CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA** mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MOR/KL/41305/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PETER JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S3772/0302** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia REBU SECONDARY SCHOOL mwaka 2012, Cheti cha kidato cha sita chenye index No. **S0101/0638** Kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia AZANIA SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARM/B1/VOL2/24/362/2018**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PETER SIGELA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S1060-0074** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. MARY'S SECONDARY SCHOOL mwaka 2002, Cheti cha kidato cha sita chenye index No. **S0125/0568** Kilchotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia LYAMUNGO SECONDARY SCHOOL mwaka 2005. Vyeti hivi vimepotea Jijini DAR ES SALAAM. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **SBR/RB/4369/2012**

## KUPOTEA KWA VYETI



**NEEMA SHOO ROBSON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S0302/0128**. Kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa mwaka 2000 ARUSHA SECONDARY SCHOOL. Cheti cha Ualimu chenye **No.e520/0141** kilichotolewa na chuo cha Ualimu Singachini Kilimanjaro mwaka 2003. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu naye . Polisi taarifa: **PHQ/ARU/ARU/32603/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**IMAN KHALID MUNIF** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TAE142776** iliyotolewa tarehe 18/07/2019 iliyotolewa uhamiaji makao makuu. Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/268690/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANDREW CHARLES MUSHUBIRWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0185/0002** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SENGEREMA SEMINARY mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi : **PHQ/DAR/KIN/268214/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JASTINE ZAKAYO REUBEN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index **No. S2354/0020** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EAGLES SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/PWA/CHA/26552/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**FATUMA OMARY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S0652/0018** Kilichotelewa na POMERINI SECONDARY SCHOOL mwaka 1999. Cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **P1862/0040** kilichotolewa na MESAC SECONDARY SCHOOL mwaka 2007. Cheti cha kidato cha sita chenye Index No. **P0438/0505** kilichotolewa na MASJD QUBAH MUSLIM SECONDARY SCHOOL mwaka 2009 .Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya **Polisi: OB/RB/6024/2013**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NYAMBURA RICHARD MSETI** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato nne chenye Index namba **S.2652/0057** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Kom SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/SHI/9811/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JANETH KENETH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne index namba. **S1280/0004** kilichotolewa na **USANGU SECONDARY SCHOOL**. mwaka **2009** yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **9910835434913/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **DAVIS ADOLF MWAMUNYANGE** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 834 DQV** aina ya **TOYOTA KLUGER** chassis namba **ACU700030815,** engine **ZA200658075.**Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/261476/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**JUMA RASHIDI LUSHINO** anatangaza kupotea kwa kadi za Pikipiki aina ya, **SANLG** yenye Usajili **T369 CZE. TOYO** yenye Usajili **MC716 AZT na SANLG** yenye Usajili **MC 557 ACC.** Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nae. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/TAN/KOR/5681/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ENOCK BERNARD MYINGA,** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 250 DUS - TVS KING.** Chassis No. **MD6M14PA4P4C01127,** Engine No **AK4CP4501095.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/5927/2024.**

## KUPOTEA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**NATHAN MATHAYO NTIBONA,** Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba **433 Kitalu "DD"**kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu Taarifa ya Polisi, **PHQ/SHI/SHI/10043/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI KIWANJA

Ndugu **OMARI IDD CHAKA** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba yenye **TITLE 6287,** eneo **BABATI MJINI/MANYARA, PLOT NO. 52, BLOCK K** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi **PHQ/MAN/BAB/9836/2024**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. ……/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late WILFRED JOSHUA NKYA of Area C Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANETH WILFRED NKYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**
……………………………………………

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 1, 2025
Date at Dodoma this 19TH Day of November, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 26190 OF 2024**
**In the Matter of the Estate of the late JABIRI MUSSA KASUBI of MUUNGANO NKUHUNGU AREA, WITHIN THE CITY AND REGION OF DODOMA**
**AND**
**In the matter of an application for Letters of administration by NEEMA LAZARO SHABANI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30 day of 12………………… 2024
Dated at Dodoma this 4 day of 12…………………2024

COURT CLERK
COURT CLERK

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU**
**Shauri la Madai Na. 213/2024**
**Jina la Mwombaji: ESTER MKOMYA**
**Jina la Mdaiwa: EMMANUEL ELIKANA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu madai katika mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: EMMANUEL ELIKANA**
**GEITA**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**"Madai ya Tsh. 2,060,000/="**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi kwa majibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 02 Mwezi 12 Mwaka 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI**
**AT KINONDONI**
**COMMERIAL CASE NO 25549 OF 2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD – PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MUSA LUCHACHE – DEFFENDANT**

**TO: MUSA LUCHACHE**
**DAR ES SALAAM**

**NOTICE OF DATE MENTION/ HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **JUDGMENT** on 10th day of DECEMBER, 2024 at 8:30am before Hon RWEHUMBIZA Resident Magistrate.
**YOU ARE HEREBY** required to appear in this court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.
**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 05th Day of DECEMBER, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI**
**AT KINONDONI**
**COMMERIAL CASE NO 2551 OF 2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD – PLAINTIFF**
**VERSUS**
**ANSILA KOMBA – DEFFENDANT**

**TO: ANSILA KOMBA**
**DAR ES SALAAM**

**NOTICE OF DATE MENTION/ HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **JUDGMENT** on 10th day of DECEMBER, 2024 at 8:30am before Hon RWEHUMBIZA Resident Magistrate.
**YOU ARE HEREBY** required to appear in this court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.
**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 05th Day of DECEMBER, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Wabunge Korea Kusini kupiga kura kumshtaki rais

**SEOUL,** Korea Kusini

WABUNGE wa upinzani nchini Korea Kusini wameazimia kupiga kura ya kumfungulia mashtaka Rais Yoon Suk Yeol kwa jaribio lake la kutangaza sheria ya kijeshi.

Hayo yanajiri wakati waziri wa ulinzi anayeshtumiwa kwa kumshauri rais huyo juu ya kutangaza sheria ya kijeshi amejiuzulu.

Msemaji wa Chama cha Democratic, alisema wabunge hao wamepanga kesho watapiga kura bungeni ya kumfungulia mashtaka Yoon.

Awali, mbunge wa chama hicho cha Democratic, Kim Seung-won, aliliambia bunge kwamba tangazo la serikali inayoongozwa na Rais Yoon ya kutumia sheria ya dharura ya kijeshi ilisababisha watu kuchanganyikiwa na kupata hofu nchini humo.

Chama tawala cha Yoon cha People Power Party, kimegawanyika kuhusu mgogoro huo, lakini kilisema kitaungana katika kura hiyo.

Chama cha Democratic kinahitaji angalau wabunge wanane kati ya 108 wa chama tawala kuunga mkono hoja hiyo ili ipitishwe na theluthi mbili ya wingi wa kura za bunge hilo lenye viti 300.

Hata hivyo, Rais Yoon Suk Yeol anakabiliwa na shinikizo la kuondoka madarakani kutoka kwenye chama chake cha People's Power Party.

Kiongozi wa chama hicho Han Dong-hoon, aliwaambia waandishi wa habari kuwa anamtaka rais huyo kujiuzulu kutoka ndani ya chama hicho.

Rais Yoon ameonekana kuendelea na kazi yake, huku akikubali kujiuzulu kwa Waziri wa Ulinzi, Kim Yong-hyun, ambaye inasemekana ndiye aliyependekeza sheria ya kijeshi kutumika.

Kim aliomba radhi kwa baraza la mawaziri hapo jana na kujiuzulu.

Hata hivyo, maandamano zaidi na mikutano ya hadhara inafanyika nchini kote, huku kuna fununu Rais Yoon anatarajia kutoa hotuba ya kuomba msamaha.

# Waziri Mkuu Ufaransa ang'olewa madarakani

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amekuwa na wakati mgumu kuumaliza mzozo wa kisiasa ulioibuka baada ya Waziri Mkuu, Michel Barnier, kuondolewa madarakani na bunge.

Barnier amekuwa waziri mkuu wa kwanza kuondolewa madarakani katika kipindi cha zaidi ya miongo sita iliyopita.

Wabunge wa Ufaransa walipiga kura ya kutokuwa na imani na waziri mkuu usiku wa Jumatano.

Saa chache bada ya tukio hilo, Waziri Mkuu Michel Barnier amewasilisha barua ya kujiuzulu ikulu ya nchi hiyo kwa Rais Macron.

Serikali ya Waziri Mkuu Barnier iliyodumu kwa miezi mitatu tu, inakuwa miongoni mwa zilizokaa madarakani kwa muda mfupi zaidi tangu mwaka 1958 na inakuwa mara ya kwanza kwa serikali kuangushwa kwa kura ya kutokuwa na imani bungeni tangu mwaka 1962.

Wabunge kutoka vyama vya siasa kali za mrengo wa kulia na kushoto waliunga mkono kuondolewa kwa Barnier kwa wingi wa kura 331 dhidi ya 288 zilizokataa.

Hatua hiyo inalitumbukiza taifa la Ufaransa katika mzozo mkubwa wa kisiasa unaotishia uwezo wa serikali kuendelea na majukumu yake.

Chanzo za mzozo huu wa kisiasa, ni mjadala wa bajeti ya mwakani ambapo wabunge walikataa muswada uliopendekezwa na Waziri Mkuu Barnier wakisema ulikuwa ukibana matumizi kwenye mfuko wa kitaifa wa misaada ya kijamii.

Hata hivyo, Barnier alikaidi na kusaini muswada huo kwa kutumia sheria inayompa mamlaka ya kufanya hivyo, kitendo kilichowakasirisha wabunge.

Baada ya uamuzi huo wa kumwondoa madarakani kutangazwa, Barnier alishukuru kupata fursa ya kuitumikia Ufaransa.

**Serikali ya Waziri Mkuu Barnier iliyodumu kwa miezi mitatu tu, inakuwa miongoni mwa zilizokaa madarakani kwa muda mfupi zaidi tangu mwaka 1958 na inakuwa mara ya kwanza kwa serikali kuangushwa kwa kura ya kutokuwa na imani bungeni tangu mwaka 1962.**

"Sasa mumefikia wakati huu wa ukweli. Hatimaye, mniruhusu niseme kuwa binafsi, ninahisi kuwa nimepata fursa ya heshima ya kuongoza kwa muda wa miezi mitatu, na bado niko Waziri Mkuu wa Wafaransa wote, na wakati wadhifa huu utafikia mwisho, labda hivi karibuni, naweza kusema kwamba hii itabaki kuwa fahari kwangu kuitumikia kwa dhati Ufaransa na Wafaransa," alisema Barnier katika hotuba yake, aliwaambia wabunge.

Wabunge wa upinzani waliopata nafasi ya kuchangia hoja hiyo, walimnyooshea kidole Barnier wakisema wakulaumiwa ni yeye mwenyewe aliyeshindwa kuwashawishi wabunge na kutilia maanani matakwa ya Wafaransa walio wengi.

Baadhi ya wabunge hao walikwenda mbali na kumtaka Rais Macron ajiuzulu wakisema utawala wake wote umepoteza imani ya Wafaransa.

Kiongozi wa chama cha siasa kali za mrengo wa kulia cha National Rally, Marine Le Pen alisema kulikuwa hakuna namna nyingine isipokuwa uamuzi huu uliofikiwa.

"Ili kuwalinda watu wa Ufaransa, hakukuwa na suluhisho jingine zaidi ya hili. Sitoi wito wa kujiuzulu kwa Emmanuel Macron. Ninachokisema ni kwamba utafika wakati, tusipochukua mkondo wa kuwaheshimu wapiga kura na kuheshimu nguvu za kisiasa na za uchaguzi, basi ni wazi kwamba shinikizo kwa Rais Macron litazidi kuongezeka. Lakini yeye pekee ndiye atakayekuwa na uamuzi na neno la mwisho," alieleza Le Pen.

**DW**




Raia wa Korea Kusini wakishikilia mabango yenye maandishi 'Tunataka Yoon Suk Yeol afukuzwe' wakati wa maandamano mjini Seoul, Korea Kusini jana. **PICHA: ALLIANCE**

# Amnesty: Israel imefanya mauaji ya halaiki Gaza

**LONDON,** Uingereza

SHIRIKA la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu la Amnesty International limeshutumu Israel kwa kufanya mauaji ya halaiki dhidi ya Wapalestina katika vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza.

Katika ripoti yake iliyotolewa jana, inaeleza madai mauaji yanayoendelea eneo hilo sawa na kuangamiza jamii ya Wapalestina.

Shirika hilo lenye makao yake mjini London Uingereza lilisema limefikia hitimisho hilo baada ya miezi kadhaa ya kuchambua matukio na kauli za maofisa wa Israel.

Amnesty ilisema kiwango cha kuzingatiwa kisheria cha uhalifu huo kilifikiwa, katika uamuzi wake wa kwanza kama huo wakati wa mzozo mkali uliohusisha utumiaji wa silaha.

Mkataba wa Mauaji ya Kimbari wa mwaka 1948, uliotungwa kufuatia mauaji ya halaiki ya Wayahudi katika mauaji yaliyofanywa na serikali ya Nazi ya Ujerumani, unafafanua mauaji ya halaiki kama ni vitendo vilivyofanywa kwa nia ya kuharibu, kwa ujumla au kwa sehemu, kikundi cha kitaifa, kikabila, ubaguzi au kidini.

Israel imekanusha mara kwa mara kwa shtaka lolote la mauaji ya halaiki, ikisema kuwa imeheshimu sheria za kimataifa na ina haki ya kujitetea baada ya shambulio la kuvuka mpaka la Hamas lilofanyika Oktoba 7, 2023 ambalo lilichochea vita.

Maofisa wa Israel hawakupatikana kutoa maoni yao kuhusu ripoti hiyo ya Amnesty International.

**BBC**

## HABARI MICHEZO

# KOCHA TAOUSSI AJIVUNIA WACHEZAJI WAKE AZAM FC

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema mafanikio anayoyapata kwenye michezo ya Ligi Kuu yanatokana na kujituma kwa wachezaji wake na kufuata maelekezo anayowapa kwenye kila mchezo.

Kocha huyo juzi ametangazwa kuwa kocha bora wa Ligi Kuu kwa mwezi Novemba akimshinda kocha wa Simba, Davids Fadlu ambaye waliingia wote fainali kuwania tuzo hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Taoussi alisema anashukuru wachezaji wake kwa kila wanachokifanya uwanjani.



"Nina wachezaji wazuri, wanajitoa kwa ajili ya timu lakini pia wamekuwa wakifuata maelekezo katika kila mchezo kwenye ligi ambayo kwa kweli ni ngumu, kila mchezo ni mgumu kutokana na maandalizi ya kila timu na kila timu inataka pointi tatu," alisema.

Alisema tuzo aliyoipata inatokana na juhudi za wachezaji wake na kupelekea kupata ushindi kwenye michezo mitatu mfululizo iliyopita.

Katika mwezi wa Novemba ambayo tuzo yake kocha bora imeenda kwa Taoussi na mchezaji bora imeenda kwa Offen Chikola wa Tabora United, Azam wamepata ushindi kwenye michezo dhidi ya Singida Black Stars (2-1), Yanga (1-0) na Kagera Suhar (1-0).

Matokeo hayo yameipaisha Azam mpaka nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 30 baada ya kucheza michezo 13 miwili zaidi ya Simba na Yanga zinazoshika nafasi ya pili na ya tatu.

Simba inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 28 ikizidiwa pointi moja na Azam huku Yanga ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi 27 ikizidiwa pointi tatu na vinara Azam.

**MAZOEZI**



Wanariadha wa timu ya Mkoa wa Dar es Salaam wakifanya mazoezi kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMC yamaliza usajili dirisha dogo

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likitarajiwa kufunguliwa, Desemba 15 mwaka huu, klabu ya KMC imesema tayari imeshamaliza usajili kabla ya dirisha hilo kufunguliwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Daniel Mwakasungula, amesema wameshaingia mikataba na wachezaji ambao wanahitaji kuwaongeza kipindi hicho na kwa sasa wanasubiri kuwatangaza tu dirisha litakapofunguliwa.

"Hivi tunavyoongea tayari tumeshasajili, kwa maana ya tumeshaingia mikataba na wachezaji tunaowakusudia, dirisha likifunguliwa ni kupeleka majina yao Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) kwa ajili ya kuidhinishwa, kama unavyojua KMC ni watu ambao tunaamini sana kwenye vijana, wanaweza wasikulipe kwa haraka lakini tunaamini kuna muda utafika tutaanza kula matunda, hivyo tumesajili wachezaji wa aina hiyo," alisema Mwakasungula.

Alisema licha ya kwamba wanataka kuongeza ubora kwenye kikosi, lakini wanafanya usajili kutokana na kukabiliwa na wachezaji wengi majeruhi.

"Tuna wachezaji wengi sana majeruhi, kuna wengine tumewapeleka hadi Misri kwa ajili ya kufanyiwa matibabu na sasa wanaendelea vizuri, kwa maana hiyo tunataka kukiongezea nguvu kikosi, ila hatutochukua wachezaji wengi," alisema Mwakasungula.

KMC inashika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 14 baada ya kucheza michezo 13.

Timu hiyo imecheza mechi saba nyumbani, ikishinda nne, sare moja na kupoteza miwili, huku mechi sita za ugenini ikishinda mmoja, sare moja na kupoteza minne.

Mwanzoni mwa msimu huu ilipoteza wachezaji wake muhimu waliotimkia timu mbalimbali, akiwemo Awesu Awesu ambaye yuko na timu ya Simba kwa sasa.

# Wanavyuo 2000 kushiriki tamasha kubwa Mbeya

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MBEYA

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na kampuni na wadau imeandaa tamasha la vyuo vikuu na vyuo vya kati Desemba 9 ambalo litawashirikisha wanavyuo zaidi ya 2000 wa mkoani Mbeya.

Miongoni mwa wadau watakaoshirikiana na ofisi hiyo ya Mkuu wa Mkoa ni pamoja na MC Edwin Luvanda Branding and Entertainment.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Edwin Luvanda akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema tamasha hilo litakuwa na kaulimbiu 'Kuelekea Miaka 30 ya Beijing Chagua Kutokomeza Ukatili' na litafanyika katika Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA) tawi la Mbeya.

tamasha hilo litaenda sambamba na maadhimisho ya uhuru wa Tanganyika.

Luvanda alisema lengo kuu la tamasha hilo ni kutangaza na kuviweka pamoja vyuo vilivyopo Mkoa wa Mbeya pamoja na kutangaza fursa za utalii zilizopo mkoani humo ili kuwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi waweze kuvitembelea.

„Wakati wa tamasha hili michezo mbalimbali itafanyika kama mpira wa miguu kwa wanawake na wanaume, mpira wa pete na kuvuta kamba," alisema Luvanda.

Aidha, aliongeza kuwa shughuli nyingine zitakazofanyika ni uchangiaji wa damu kwa hiari na huduma ya upimaji magonjwa mbalimbali kwa hiari.

Mkurugenzi huyo amewaomba wanavyuo na wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa ujumla kujitojkeza kushiriki tamasha hilo ambalo ni la muhimu sana katika kuutangaza Mkoa huo.

Kampuni hiyo imekuwa ikiandaa shughuli mbalimbali kwa mikoa ya nyanda za juu ambapo mwezi Oktoba 2024 iliandaa Usiku wa Dhahabu hafla ambayo iliwashirikisha wachimbaji madini kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CUNHA ATAKIWA ARSENAL**
ARSENAL imefanya mazungumzo ya awali na mshambuliaji wa Wolves na Brazil, Matheus Cunha mwenye umri wa miaka 25. (***Caught Offside***)

**VAN DIJK NA MKATABA MPYA**
BEKI wa Uholanzi, Virgil van Dijk amepokea ofa ya mkataba mpya kutoka kwa Liverpool lakini haiendani na matarajio ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 33. (***Athletic***)

**LOPETEGUI MAMBO MAGUMU**
MUSTAKABALI wa Julen Lopetegui kama kocha mkuu wa West Ham uko shakani. (***Sky Sports)***

**RODRI KUMVUTA NICO CITY**
RODRI ameiomba Manchester City kumnunua mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22 kutoka Athletic Bilbao. (***Metro)***

**KLABU ZAMTAKA MAGUIRE**
MLINZI wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 31 anawaniwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England huku mushtakabili wake kule Manchester United ukiwa haujulikani. (***Football Insider***)

**ENRIQUE HAMTAKI GYOKERES**
KOCHA wa PSG, Luis Enrique hataki klabu hiyo ya Ufaransa kumsajili mshambuliaji wa Sporting na Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester City na Manchester United. (***Foot Mercato)***

**NEWCASTLE YAMUWINDA SEMENYO**
KLABU ya Newcastle United inawafuatilia winga wa Bournemouth na Ghana, Antoine Semenyo mwenye umri wa miaka 24 na mshambuliaji wa Brentford na Cameroon, Bryan Mbuemo mwenye umri wa miaka 25. (***The i News***)

**PEC AZIVUTIA ARSENAL, L'POOL**
ARSENAL na Liverpool zinamfuatilia winga wa LA Galaxy mwenye umri wa miaka 23 kutoka Brazil, Gabriel Pec. (***Caught Offside)***

**SELLES ATAJWA HULL CITY**
KLABU ya Hull City inatazamia kumteua kocha wa Reading, Ruben Selles kama kocha wao mpya, huku Alex Neil na Slavisa Jokanovic wakiwa miongoni mwa wengine wanaowania nafasi hiyo. (***Telegraph***)

**CUMMINGS LULU ENGLAND**
KLABU za Ligi Kuu England zinamfuatilia mshambuliaji wa Celtic mwenye umri wa miaka 18, Daniel Cummings. (***Mail)***

**BROWNLIE ATAKIWA CRYSTAL**
KLABU ya Crystal Palace inatazamiwa kumsajili mshambuliaji wa Australia, Rylan Brownlie mwenye umri wa miaka 17 kwa uhamisho wa bure. (***Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK, LIVERPOOL BADO HAKIELEWEKI

## ●●●Licha ya klabu hiyo kumpa mkataba mpya lakini bado wameshindwa ku...

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imempa beki wa kati Virgil van Dijk mkataba mpya, lakini imeshindwa kutimiza matakwa ya Mholanzi huyo, kwa mujibu wa Dail Mail.

Van Dijk ni mmoja wa nyota watatu wanaokaribia miezi sita ya mwisho ya mikataba yao pamoja na Trent Alexander-Arnold na Mohamed Salah, ambaye amefichua hadharani kuwa bado hajapewa ofa mpya.

Haionekani kuwa hivyo kwa Van Dijk, hata hivyo ripoti inasema Liverpool imempa beki huyo wa Uholanzi ofa ya kuendelea kusalia Anfield.

**Ofa hiyo inasemekana haikufikia matarajio ya Van Dijk linapokuja suala la mshahara na muda.**

Muhimu zaidi, mazungumzo bado yanaendelea kati ya Liverpool na wawakilishi wa Van Dijk kutafuta makubaliano.

Beki huyo amekuwa akijibu maswali mara kwa mara kuhusu mustakabali wake hadharani wakati mazungumzo yakiendelea.

Uongozi wa klabu hiyo ya Merseyside pia wanatarajiwa kutoa ofa rasmi kwa Salah, ambaye anaaminika kuwa na furaha kusaini nyongeza ya mwaka mmoja iwapo itatolewa.

Wakati huo huo, Liverpool pia wapo kwenye mazungumzo ya dhati na beki wa kulia Alexander-Arnold, ambaye anawindwa na Real Madrid, lakini hitimisho la sakata hili linaloendelea bado haliko wazi.

Kiungo Alexis Mac Allister hivi majuzi aliitaka Liverpool kuharakisha makubaliano na Van Dijk, Salah na Alexander-Arnold, akisisitiza kuwa kikosi hicho kina nia ya kuendelea kucheza pamoja na wachezaji hao watatu kwa miaka ijayo.

# AMORIM ALIA UFITI WA WACHEZAJI MAN UNITED



**LONDON,** England

RUBEN Amorim amesema alilazimika kufanya kazi kwa muda mfupi na wachezaji wake waliorejea kutoka kuwa majeruhi wakati Manchester United alipopata kipigo chake cha kwanza akiwa kocha klabu hiyo wakichapwa 2-0 na Arsenal Jumatano.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Jurriën Timber na William Saliba yaliipa ushindi Arsenal na kupeleka kichapo cha kwanza kwa kocha huyo wa zamani wa Sporting CP.

Lakini huku kikosi cha United kikiwa bado kimetatizwa na majeraha, Amorim alisema uteuzi wake unaendelea kuathiriwa na wasiwasi wa utimamu wa mwili wa wachezaji wake.

Harry Maguire, Tyrell Malacia na Mason Mount wote walicheza pale Emirates baada ya kurejea hivi karibuni kutoka kwenye majeruhi, huku Leny Yoro aliyesajiliwa majira ya joto akiichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kuumia mguu kwa muda mrefu.

"Sio kwa sababu napenda kubadilika kila wakati, lakini lazima tuwe na kikosi kizima," alisema Amorim.

"Kwa mfano, Harry Maguire ana kikomo cha wakati, Tyrell Malacia ana kikomo cha wakati, Mason Mount ana kikomo cha wakati, Leny Yoro ana kikomo cha wakati, kwa hiyo tunapaswa kusimamia ndani ya michezo kwa mbinu tofauti.

"Tunapaswa kutathmini na watu ambao wako katika hatari kidogo ya majeraha hawatacheza, kwa hiyo lazima tuwe na kila mtu kufanya kazi, kucheza na kuboresha kikosi."

Licha ya kushindwa, Amorim alisema bado atapata matokeo chanya kutokana na uchezaji wa wachezaji wake pale Emirates.

"Nafanya tathmini ya mchezo bila kujali matokeo," alisema.

"Kama nilivyosema, baada ya ushindi wa 4-0 dhidi ya Everton unaweza kuchukua mambo chanya, lakini lazima tuboreshe na tayari tulijua hilo."

# Guardiola: Ilikuwa lazima Man City ishinde



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City ilimaliza wakati wake mgumu wa kucheza mechi saba mfululizo bila kushindi kwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Nottingham Forest na Pep Guardiola alisherehekea na kusema ni hatua muhimu ya mabadiliko.

"Tulihitaji," alisema kocha huyo wa City, ambaye pia alimaliza matokeo yake mabaya zaidi katika maisha yake ya kufundisha.

"Jambo muhimu zaidi lilikuwa ni kuvunja utaratibu huu wa kutoshinda michezo na hatimaye tukashinda, lakini lazima tuendelee.

"Klabu, wachezaji, kila mtu alihitaji kushinda. Baada ya matukio ya hivi karibuni, hatukuwa tumepumzika hadi kipenga cha mwisho."

Kurudi kwa Kevin De Bruyne kwenye kikosi cha mwanzo kulidhihirishwa na utendaji mzuri.

Mbelgiji huyo akafunga bao na kusaidia jingine, na kutawala juhudi za mashambulizi ya City katika mchezo wake wa kwanza baada ya miezi miwili.

Hata hivyo, Guardiola alionya kuhusu utimamu wa kiungo huyo.

"Siku tatu, tutaona jinsi De Bruyne anahisi," alisema Guardiola.

Beki wa City, Nathan Aké alilazimika kutoka nje mwishoni mwa mchezo kutokana na jeraha la misuli ya paja, hali inayotia wasiwasi kutokana na kutokuwepo kwake kwa muda wa wiki tano msimu huu.

"Nathan haonekani vizuri. Tutatathmini hali kesho," alisema Guardiola.

"Hakuweza kuendelea, na tutajua zaidi baada ya siku tatu. Nimesikitishwa na Nathan."

Manuel Akanji pia alikosekana katika kipindi cha pili kutokana na jeraha, ingawa Guardiola alionesha kuwa hali haikuwa mbaya sana.

# Mbappé atabiriwa kufanya vizuri zaidi

**SAN MAMES,** Hispania

KOCHA Carlo Ancelotti amesisitiza kwamba, Kylian Mbappé anaweza kufanya vizuri zaidi baada ya kukosa penalti yake ya pili ndani ya wiki moja wakati Real Madrid wakichezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Athletic Club Jumatano kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania.

Álex Berenguer aliiweka Athletic mbele dakika ya 53 pale San Mamés, na Mbappé alipata nafasi ya kusawazisha dakika 15 baadaye, lakini mkwaju wake wa penalti uliokolewa na kipa Julen Agirrezabala.

Jude Bellingham kisha akasawazisha kabla ya Gorka Guruzeta wa Athletic kufunga bao la ushindi kutokana na makosa ya Federico Valverde.

Kushindwa kwa Mbappé kufunga penalti hiyo kulikuja wiki moja baada ya kuona juhudi nyingine iliyookolewa na Caoimhín Kelleher wa Liverpool wakati wakipoteza 2-0 kule Anfield kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Sijazungumza na Mbappé," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Sipaswi kutathmini mchezo wa mchezaji kulingana na penalti. Wakati mwingine unawafunga, wakati mwingine haufungi. Ni wazi kuwa ana huzuni na kukata tamaa, lakini lazima tuendelee."

"Fede Valverde ana huzuni na amekatishwa tamaa kama Kylian, lakini Fede ni mchezaji mzuri. Watu hufanya makosa katika soka."

Mbappé amefunga mabao 10 katika mechi 20 alizochezea Madrid hadi sasa, lakini amekabiliwa na ukosoaji mkubwa juu ya kiwango chake mwezi uliopita na alichukua lawama zote za matokeo kwenye mitandao ya kijamii.

"Matokeo mabaya. Kosa kubwa katika mechi ambapo kila jambo lina umuhimu," aliandika Mbappé.

"Nachukua jukumu kamili kwa hilo. Wakati mgumu lakini ni wakati mzuri wa kubadilisha hali hii na kuoyesha mimi ni nani."

Ancelotti alisema kwamba Mbappé ataendelea kuwa mpigaji penalti kwa Madrid, pamoja pamoja na Vinícius Júnior na Bellingham.

"Hayuko katika kiwango chake bora, lakini inabidi tumpe muda wa kuzoea," alisema kocha huyo wa Madrid.

"Amefunga mabao 10, anaweza kufanya vizuri zaidi, na anajitahidi kufanya vizuri zaidi."

Kipigo hicho kinaifanya Madrid kuwa pointi nne nyuma ya vinara wa LaLiga Barcelona wakiwa na mchezo mmoja mkononi.



# Yanga yafanyiwa figisu Algeria

INATOKA UKURASA 24

dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Al Hilal ndio kinara wa Kundi A, ikifuatiwa na MC Alger, TP Mazembe na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanaburuza mkia.

Wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba nao wako Algeria na kesho watashuka dimbani kuwavaa wenyeji, CS Constantine, katika mechi ya michuano ya Kombe la Shirikisho.

# Simba SC kamili, hawahofii baridi

INATOKA UKURASA 24

wasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia Nipashe kutoka nchini humo, safari yao ilikuwa nzuri na hawajakutana na changamoto ya aina yoyote.

"Tunashukuru tumefika salama ingawa tuliingia usiku, Kocha Fadlu ameandaa programu yake ya mazoezi ambayo itaanza leo (jana) saa tisa, kila kitu kipo salama kabisa, Wana-Simba wasiwe na wasiwasi," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo waendelee kuiombea dua njema timu yao ifanye vizuri katika mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Mchezo huo unatarajia kutoa kinara wa kundi hilo kutokana na timu zote kupata pointi tatu katika mechi iliyopita, Simba ikiwafunga Bravos do Maquis ya Angola bao 1-0 na CS Sfaxien ya Tunisia ikivuna ushindi kama huo dhidi ya CS Constantine.

Katika mechi hiyo, Simba itamkosa kipa wake mzoefu, Aishi Manula, ambaye aliugua ghafla la kulazimika kubakia nchini.

Makipa wawili waliosafiri katika kikosi cha Wekundu wa Msimbazi ni Moussa Camara, raia wa Guinea na Mtanzania Ally Salim.



# COASTAL YAJIWEKA PEMBENI USAJILI WAPYA DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imesema haitasajili na haitaacha mchezaji yoyote kipindi cha dirisha dogo la usajili, imethibitishwa.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Omary Ayoub, aliliambia gazeti hili jana uamuzi huo umetokana na mwenendo wa timu yao katika michezo mbalimbali ya ligi hiyo inayoendelea hapa nchini.

Ayoub alisema hawaoni sababu ya kuongeza mchezaji kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa rasmi ifikapo Desemba 15, mwaka huu kwa timu mbalimbali kuanza mchakato wa kuongeza nguvu katika vikosi vyao.

"Timu yetu inaendelea vizuri na tunaridhishwa na matokeo tunayoyapata, mwenendo wa mwalimu na wachezaji unaturidhisha kabisa. Ni kweli tunakwenda kipindi cha dirisha dogo la usajili, lakini sisi hatutegemei mabadiliko yoyote kwenye kikosi chetu, tunaamini kazi inayofanyika sasa ni nzuri, hatuna mpango wa kuingiza wala kupunguza," alisema Ayoub.

Katibu Mkuu huyo alitaja sababu ya kutosajili ni kikosi chao kupata matokeo mazuri katika michezo ya Ligi Kuu kwa sasa na hata kama wanapoteza, basi ni kwa sababu za kimbinu za kisoka, lakini si ubora wa wachezaji, mwalimu, wala uzembe.

"Timu inaendelea vizuri, tunapata matokeo mazuri, kama tunapoteza basi ni kawaida tu ya mpira wa miguu, michezo ya nyumbani ambapo tupo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha tunashinda.

Coastal Union ni wenyeji wa ligi hakuna changamoto mpya au za ajabu sana tofauti na misimu iliyopita, hatutasajili wala kumtoa mchezaji kwenda timu nyingine kwa mkopo kwa sababu tutakuwa tunajipa udhaifu wenyewe," aliongeza.

Kauli hii inazima tetesi kuhusiana na timu hiyo kuhusishwa na taarifa za kutaka kumuuza beki wake, Lameck Lawi, ambaye imeripotiwa anatakiwa na Yanga kipindi hiki cha dirisha dogo baada ya dili lake la kujiunga na Simba kushindikana.

Coastal Union ambayo msimu uliopita ilimaliza nafasi ya nne na kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikatolewa hatua za awali na Bravo do Maquis ya Angola.

Kwa sasa mabingwa hao wa Ligi Kuu mwaka 1988 wako katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wakiwa na pointi 16, ikicheza mechi 13, ikishinda mara nne, kutoa sare nne na kupoteza michezo mitano.

Imeshinda mechi nne kati ya saba ilizocheza nyumbani, ikipoteza tatu, huku ikiwa haijashinda hata mchezo mmoja kati ya sita iliyocheza ugenini mpaka sasa, ikitoa sare nne na kupoteza miwili.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 15 wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano ya Afrika (CAF U-15), kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika kuanzia keshokutwa jijini Kampala, Uganda. **PICHA: TFF**

# Serikali yafuta uchaguzi TOC

**Na Somoe Ng'itu**

SERIKALI imetangaza kuufuta uchaguzi mkuu wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), uliotarajiwa kufanyika Desemba 28, mwaka huu jijini Dodoma.

Awali uchaguzi mkuu wa TOC ulipangwa kufanyika Desemba 14, mwaka huu jijini humo.

Rais wa TOC, Gulam Abdullah Rashid, alisema jana jijini kamati yake imepokea taarifa ya kufutwa kwa uchaguzi huo na Kaimu Msajili wa Vyama vya Vilabu vya Michezo Nchini.

Gulam alisema uamuzi huo umetokana na malalamiko yaliyopelekwa kwa msajili na hivyo wao wanatekeleza mwongozo walioupokea.

Alisema baadhi ya malalamiko yaliyowasilishwa ni kuanza kwa mchakato wa uchaguzi kwa kutumia katiba ambayo ilikuwa haina ithibati ya Msajili.

"Kamati ya Olimpiki pamoja na kutopokea malalamiko kutoka kwa wanachama wake, inaridhia kuufuta mchakato huo na utalifikisha katika mkutano wake mkuu utakaofanyika Desemba 28, 2024 mjini Dodoma ili kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi," ilisema sehemu ya taarifa ya Gulam.

Nafasi ya Urais wa TOC inawaniwa na Michael Washa, Anthony Mtaka na Henry Tandau kutoka Tanzania Bara wakati mgombea pekee wa nafasi hiyo ni Nassra Mohammed.

Michezo

Nipashe Ijumaa Desemba 6, 2024



Mbappé atabiriwa kufanya vizuri zaidi

UKURASA 22

# Yanga yafanyiwa figisu Algeria

## ●●● Vigogo hao wa Jangwani wasema mambo yote uwanjani...

**Na Adam Fungamwango**

MSAFARA wa Yanga 'umesoteshwa' kwa saa nne kwenye Uwanja wa Ndege baada ya kuwasili nchini Algeria kwa ajili ya kucheza mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji MC Alger itakayofanyika kesho jijini Algiers.

Mechi hiyo ya Kundi A itachezwa kwenye Uwanja wa Juillet 5 kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Kikosi cha Yanga kiliwasili salama nchini humo lakini kililazimika kutumia zaidi ya saa nne kwenye uwanja wa ndege ili kukamilisha taratibu za uhamiaji na kusubiri mizigo yao na kuanza safari ya kuelekea hotelini.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, Alex Ngai, alisema kwa kile walichokikuta na kukipata uwanjani, ni ishara mechi ya mpira wa miguu dhidi ya wapinzani wao imeanza rasmi nje ya uwanja.**

Ngai alisema walishangazwa kuona ucheleweshaji wa kukamilisha taratibu za uhamiaji na kusababisha kutumia muda mrefu wakiwa uwanjani hapo.

"Kiukweli mechi imeanza rasmi, tumefika saa sita usiku, lakini hadi kutoka hapa uwanja wa ndege tumetumia kama saa nne, tumetumia saa mbili kwenye masuala ya uhamiaji, mawili mengine kusubiria mizigo yetu, lakini tunashukuru mwisho wa yote mizigo mingi imepatikana, bado michache ambao meneja anaendelea kuifutilia nina imani ataipata.

Nadhani sasa mechi ya mpira wa miguu iliyotuleta hapa Algiers imeanza rasmi nje ya uwanja, hatukutarajia, lakini tulijipanga kwa sababu mechi hizi za Kiafrika zina matatizo sana, wala hii haitatutoa mchezoni, tuna viongozi na wachezaji ambao ni wazoefu katika michezo kama hii ya kimataifa," alisema Ngai.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema walitumia saa saba kutoka Dubai hadi Algiers, kabla ya kukutana na saa nne nyingine uwanja wa ndege.

Kamwe alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na changamoto hiyo waliyokutana nayo ni ya kawaida na haiwaondoi kwenye malengo ya kusaka ushindi hapo kesho.

"Hebu angalia hapo, tumetumia zaidi ya saa 10, kutoka Dubai hadi hapa, yote kwa yote tumekuja katika mapambano, baada ya kuanza vibaya kwa kufungwa, mchezo huu wa pili hatutaki kupoteza, tumekuja kwa ajili ya kulinda heshima ya klabu yetu ya Yanga," alisema Kamwe.

Kuhusu hali ya baridi, Kamwe alisema waliamua kwenda mapema nchini huko ili kuzoea hali hiyo.

"Daktari wetu alisema kama tutatumia zaidi ya saa 48, itatusaidia kuzoea hali ya hewa, na hichi ndio tulichokifanya kuhakikisha tunakuja (Algeria), mapema," aliongeza ofisa huyo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sead Ramovic, jana aliwafanyisha wachezaji wake mazoezi ya kuweka miili sawa baada ya safari ndefu.

"Mazoezi haya ya leo (jana), ni ya kuweka miili ya wachezaji sawa, tutakuwa tunafanya majira ya saa 2:00 usiku kwa saa za hapa kwa sababu ni muda ambao mechi yetu itachezwa, sababu nyingine ni kuzoea hali ya hewa maana baridi huku ni kali sana," alisema kocha huyo.

Yanga ilianza hatua hiyo ya makundi kwa kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Al Hilal Omdurman ya Sudan, mechi iliyochezwa Novemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati MC Alger ililazimisha suluhu ya ugenini

INAENDELEA UK. 23



Pacome

# Simba SC kamili, hawahofii baridi

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuwasili salama nchini Algeria, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema hali ya hewa ya baridi kali si tatizo kwa wachezaji wake ambao wamekwenda kuivaa CS Constantine katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa.

Mechi hiyo kati ya CS Constantine na Simba itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Akizungumza kwa njia ya simu kutoka katika mji wa Constantine, Fadlu, alisema wamewasili salama huku wachezaji wake wakiwa katika hali nzuri licha ya kukutana na hali hiyo ya baridi kali.

"Tupo vizuri, nadhani leo (jana), saa tisa (sawa na saa 11 jioni kwa Tanzania), kwa saa za huku tutafanya mazoezi yetu ya kwanza, naamini kwa siku hizi mbili wachezaji watazoea hali ya hewa ya hapa," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema mazoezi waliyofanya jana na ya mwisho yatakayofanyika leo yatampa picha kamili ya kikosi chake kuelekea mchezo huo wa pili wa hatua ya makundi.

"Baada ya mazoezi ya leo (jana) tutafanya tena mazoezi kwenye uwanja rasmi ambao tutakaotumia kucheza mechi, hayo yatakuwa mazoezi muhimu sana kwetu kuelekea siku ya mchezo, kwa sasa nafurahia hali ya wachezaji wangu, kila mmoja na anautamani mchezo huu," alisema Fadlu.

Naye Meneja wa Habari na Ma-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >